# Mazungumzo ya Mwislamu na Mkristo

**H. M. Baagil, M. D.**

**WAMY Studies on Islam**

## YALIYOMO

Muhtasari wa Mtunzi ........ 4
Utangulizi ........ 6
MAZUNGUMZO ........ 8
Biblia Takatifu ........ **Error! Bookmark not defined.**
Imani ya Utatu ........ **Error! Bookmark not defined.**
Imani ya Uungu wa Yesu Kristo ........ **Error! Bookmark not defined.**
Imani ya kuamini Uungu Mwana wa Yesu ........ **Error! Bookmark not defined.**
Je, Yesu amesulubiwa? ........ **Error! Bookmark not defined.**
Imani ya Mateso, Kifo cha Yesu na Dhambi ya Asili . **Error! Bookmark not defined.**
MUHAMMAD KATIKA BIBLIA ........ **Error! Bookmark not defined.**
Kigezo cha Mtume na Yeremia ........ **Error! Bookmark not defined.**
Hadi atakapokuja Shiloh (Yeye Mwenye Amani) **Error! Bookmark not defined.**
Baka ni Maka ........ **Error! Bookmark not defined.**
Nyumba ya Utukufu Wangu ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mpanda Punda na Mpanda Ngamia ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mtume Kama Musa ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mtumishi wangu, Mjumbe na Mteule ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mfalme Daudi Alimwita Huyo “Bwana Wangu” ........ **Error! Bookmark not defined.**
Wewe U Nabii Yule? ........ **Error! Bookmark not defined.**
Kubatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto ........ **Error! Bookmark not defined.**
Mdogo Katika ufalme wa Mbinguni ........ **Error! Bookmark not defined.**
Msaidizi ........ **Error! Bookmark not defined.**
Ufunuo kwa Mtume Muhammad ........ **Error! Bookmark not defined.**
Marejeo ........ **Error! Bookmark not defined.**

## Shukrani

Mimi ni Mmarekani niliyekulia katika imani ya Kikristo tangu utotoni. Mpaka pale nafsi yangu ilipoanza kuuliza kuhusu Mungu, nimefanya mambo mengi ya muhimu sana ili niyatoe kwa watu.

Baada ya kukijadili, kukisoma, na kukisoma tena kitabu hiki cha Mazungumzo ya Mwislamu na Mkristo, na kuzirejea nukuu kutoka katika Biblia Takatifu ya King James Version na Qurani Takatifu.

Hatimaye natangaza shahada yangu (ushuhuda) hadharani kwa Kingereza, kisha kwa Kiarabu: Nashuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah, Asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mtumishi wake na ni nabii wake. (Ashhadu an la illaha illa Allah, wahdahu la sharikah lahu, wa ashhadu anna Muhammad abduhu wa rasulahu).

Kwa kupitia ushuhuda huu wa msingi na mwepesi mno, ninaamini watu wengi watamtii Allah kiroho na kweli.

Nataraji kuwa kijitabu hiki kifupi na chepesi kukisoma kitasomwa ulimwenguni kote na kitawavutia wengi miongoni mwa wanaotafuta imani ya kweli, nyoyo zao zitapata kutulia na kutosheka kwa kitabu hiki.

**Roy Earl Johnson**

## Muhtasari wa Mtunzi

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

Kitabu hiki kimeandikwa kikiwa ni matokeo ya mazungumzo niliyoyafanya na viongozi wa Kikristo na walei[1]. Majadiliano yalikuwa ya upole, furaha, kirafiki na yenye maoni ya kujenga, bila ya chembe ya kukusudia kuumiza (kukashifu) hisia za kidini za Mkristo yoyote. Nayo ni mazungumzo ya kuuchangamsha na kuupa changamoto Ukristo. Hayo ni mazungumzo ya lazima kwa wale wanaotafuta ukweli na kwa wale wanaojifunza mlinganisho wa dini.

C: Mkristo
M or m: Mwislamu
(SAW): Rehema na amani ziwe juu yake
(AS): Mungu Amrehemu au Amani iwe juu yake, Amani iwe juu yao

(Hizo herufi ni vifupisho vya tungo (sentesi) zinazosemwa na Waislamu wote baada ya kutajwa jina la mtume yoyote. Herufi hizo zitatumika katika kitabu hiki).

H. M. Baagal, M. D.

Januari 1984

[1] Wakristo wa kawaida.

## Utangulizi •

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

Namshukuru Allah kwa kunipa nafasi ya kukisoma kitabu Mazungumzo ya Mwislamu na Mkristo na kuombwa niandike utangulizi wa kitabu hiki kinachofumbua macho bila kifani. Mtu yoyote mwenye shauku ya kulinganisha dini atakuta katika kitabu hiki maajabu mengi yanayotoa changamoto kwa kile kilichoaminiwa na watu wengi hapo kabla kuwa ni ukweli usio na shaka.

Kazi hii ya Dr. Hasan M. Baagil inaakisi uangalifu na bidii zake za kuwasilisha matokeo aliyoyapata kwa uwazi, muhtasari, na kikamilifu. Kikiwa ni matokeo ya uchunguzi wake juu ya Ukristo na Biblia kwa zaidi ya kipindi cha miaka minne, Dr. Baagil, Mwislamu aliyejitolea, amejifunza kuwa Wakristo wanatofautiana katika misingi ya imani zao (yaani, Utatu, Uungu wa Yesu, nk.), kiasi ambacho imani ya Kanisa mara nyingi inapingana na Biblia, na hata Biblia inajipinga yenyewe! Mazungumzo yake na kiongozi na walei wa Kikristo katika kipindi hiki cha uchunguzi yamethibitisha msukumo wa kuwepo Mazungumzo Ya Mwislamu na Mkristo.

Msomaji atashangazwa kugundua kuwa, katika Biblia, Yesu (AS) kamwe hajadai kuwa yeye ni Mungu; hajakufa msalabani; na miujiza iliyofanywa naye, pia ilifanywa na mitume wengine wengi, hata makafiri nao waliifanya, na kuwa Yesu mwenyewe alitabiri kuja kwa Mtume Muhammad, rehema na amani ziwe kwao. Yote haya ukijumulisha na mengine mengi yameelezwa kwa maelezo kamili, yaliyo machache, yaelezayo kwa uwazi na yenye maana pana ya maandiko ya Biblia. Swali ambalo kwa uwazi kabisa lazima liibuke baada ya kuyatolea ushahidi hayo makinzano ya wazi nalo ni: Je, Biblia ni Neno la Mungu? Juhudi za Dr. Baagil kwa hapa, si kukusudia kuwakashifu Wakristo, na bila shaka si kumdhihaki Yesu na mafundisho yake, kwa kuwa Allah ameharamisha matendo hayo. Lengo ni kuonyesha madai ya uongo, uwasilishaji mbaya na uongo wa papo kwa papo dhidi ya Allah na Mitume yake, yote mawili: kuwakejeli na kuwadhihaki kimaumbile yanawarudia wao wenyewe.

Mazungumzo ya Mwislamu na Mkristo vilevile, kinadhihirisha mtazamo wa Kiislamu na kuonyesha namna ilivyofunuliwa Qurani kwa Mtume Muhammad miaka mia sita baada ya Yesu, rehema na amani ziwe juu yao wote wawili, inasahihisha makosa yaliyotambaa, (kwa kujua au bila kujua), ndani ya ujumbe ulioletwa na Yesu. Kitabu hiki kinatakiwa kiwe rasilimali yenye thamani sana kwa Waislamu na Wakristo, hasa hasa

wale wenye shauku ya mazungumzo kati ya imani mbili hizi. Mungu anataka, kiwe ni nyenzo ifanyayo kazi sana kwa Waislamu katika juhudi zetu za kuwaita Wakristo katika Uislamu. Kinyume chake, Wakristo kwa hakika, wanatakiwa wawe macho zaidi na kile kisemwacho na Biblia na kulichofundishwa na Yesu (AS), ikiwa ni matokeo ya kujifunza kitabu hiki. Kwa hakika, nikiwa ni Mwislamu, matarajio ni kuwa wasio Waislamu wataukubali ukweli na kuushuhudia umoja wa Allah na kuwa Muhammad ni Mtumishi na Mjumbe wake.

Allah mpe thawabu Dr. Baagil kwa juhudi zake za kuondosha giza. Allah atujaalie amani sisi sote.

**Muhammad A. Nubee**

## MAZUNGUMZO

### Mkutano Wa Kwanza Kati Ya Mkristo Na Mwislamu

C. Kwa nini kumekuwa kunaendeshwa mijadala mingi kati ya Wakristo na Waislamu kuhusu imani zao, katika muongo wa hivi karibuni?

M. Nadhani kwa sababu sote tuna vitu vingi tunavyoshirikiana. Tunamwani Muumba Mmoja Aliyetuma Mitume wengi na tunaamini kuwa Yesu ni Masihi, na ni Neno la Mungu aliyepingwa na Wayahudi. Qurani yetu inataja katika 3:45

> **"(Kumbukeni) waliposema Malaika: "Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kumzaa mtoto bila mume, bali kwa kutamkwa) Neno tu litokalo Kwake (la kukwambia 'Zaa' ukazaa pasina kuingiliwa). Jina lake ni Masih, Isa, mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu".**

Mazungumzo yameshafanywa kila mahali Ulaya, Canada, Marekani na Australia. Hata Vatican imeshirikishwa, kumeshafanyika majadiliano kati ya wanateolojia[2] wa Vitican na wanazuoni wa Kiislamu wa Kimisri mjini Rome mwaka 1970, na mjini Cairo 1974, na 1978. Mfululizo mwingine wa majadiliano kati ya wanateolojia wa Vitican na wanazuoni wa Kiislamu wa Saudia yameshafanyika huko Rome mwaka 1974. Pia Waislamu wameshaalikwa na makanisa mengi wakauwasilishe Uislamu.

C. Kama Ukristo unakaribia umri wa miaka elfu mbili na Uislamu ni zaidi ya miaka elfu moja na mia nne, kwa nini mazungumzo haya hayakufanyika katika karne zilizopita?

M. Kwa karne nne au tatu zilizopita, nchi nyingi za Asia na Afrika zilizokuwa zikitawaliwa na Waislamu zilikuwa chini ya ukoloni wa Kingereza, Kifaransa, Kiholanzi, Kibelgiji, Kihispania na Kireno. Misheni[3] nyingi za Kikristo na wafuasi wa dini wa kikoloni zilijaribu kuwabadili Waislamu wengi wawe Wakristo kwa kiasi wawezacho kwa kutumia njia yoyote ile waliyonayo: kutoa matibabu, nguo, na chakula kwa masikini. Hata hivyo, ni wachache sana waliobadili. Sehemu ndogo ya watu ilibadilika na kuingia Ukristo kwa sababu ya imani yake ya kuamini kuwa Ukristo umeleta ustaarabu na maendeleo. Wao walilikubali wazo hili potofu kwa kuwa waliamini kuwa maendeleo ya mfumo wa

---

[2] Wataalamu wa dini, Wanazuoni, Mashehe.
[3] Wajumbe wa kuuneza Ukristo.

Kimagharibi yamepatikana baada ya kuenea kwa serikali za kikanisa huko Ulaya.

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, maelfu ya Waislamu wa nchi za Asia na Afrika walihamia Magharibi wakiwa ni wafanyakazi na vibarua. Jambo lilowapelekea wawe na mahusiano makubwa na Wakristo. Pia, wanafunzi wa Kiislamu walikuwa ni watendaji katika kuutambulisha Uislamu.

C. Je, unaona kuna sababu nyingine yoyote kwa nini mazungumzo mengi yanafanyika siku hizi, hata na misheni zinazoheshimika?

M. Nadhani mwanya kati ya pande mbili hizi unakuwa mdogo zaidi, kwa vile, kila moja inaongeza uvumilivu, ingawa zote mbili bado zinashindania kupata wafuasi wengi wanaobadili dini na kuwafuata. Bado ninamkumbuka mwalimu wangu wa Ukristo, aliyekuwa anasema: “Muhammad ni tapeli, ana ndoto (za alinacha), ana kifafa.” Kwa sasa unapata maandiko machache yanayousema Uislamu kwa njia hiyo.

Sisi Waislamu, tunahisi kuwa tuna ukaribu zaidi na Wakristo kuliko Wayahudi, na wapagani, kama Qurani ilivyotabiri katika Sura 5:82:

**"Hakika utawakuta walio maadui zaidi kuliko watu (wengine) kwa Waislamuni Mayahudi na wale mushirikina (wasiokuwa na Kitabu), na utawaona walio karibu kwa urafiki na Waislamu ni wale wanaosema: "Sisi ni Wakristo. (Hayo) ni kwa sababu wako miongoni mwao wanavyuoni na wamchao Mungu, na kwa sababu wao (Wakristo) hawatakabari; (wakiijua haki huifuata).”**

Baadhi ya madhehebu ya Kikristo yanafanya maendeleo makubwa sasa hivi, kwa kutambua kwa mara ya kwanza katika historia, kuwa Muhammad (SAW) ni mjukuu wa Ismail, kwa kupitia mtoto wake wa pili; Kedar. Kamusi ya Biblia ya Davis (1980), iliyodhaminiwa na Bodi ya Elimu ya Wakristo ya kanisa la Presbyterian la Marekani, imeandika chini ya neno “Kedar” **“Mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli, ni Nebayothi, na Keadar,....** (Mwanzo 25:13) Watu wa Kedar walikuwa ni Pliny`s Cedrai, na kutokana na kabila lao hatimaye, ametokea Muhammad.) Ensaiklopidia ya Biblia ya The International Standard imenukuu yafuatayo kutoka kwa A. S. Fulton: "... Kwa Makabila ya Ismail, Kedar lazima atakuwa ni mmoja wa watu muhimu sana, na kwa hiyo katika muda uliofuata jina hilo limekuwa linatumika na makabila yote ya mabedui wa jangwani. "Ni kwa kupitia Kedar (Kwa Kiarabu – Keidar) kuwa elimu ya ukoo wa Mwislamu inafuata kizazi cha Muhammad kutoka kwa Ismail."

Vilevile kamusi ya Biblia ya Smith inachapisha yafuatayo: "Kedar, (mweusi). Mtoto wa pili wa Ismail (Gen. 25:13) ... Muhammad alifuata mstari wake kuelekea kwa Ibrahimukwa kupitia kabila tukufu la Makureishi, ambalo limechipuka kutoka kwa Kedar. Warabu wa Hijazi[4] wanaitwa Bani Harbi (wana vita), na ni wana wa Ismail, tangu mwanzoni. Palgrave anasema lugha yao ni safi kwa sasa kama ilivyokuwa wakati wa kuandikwa Qurani (AD. 610), imesalia bila ya kubadilishwa kwa zaidi ya miaka 1200; ni uthibitisho mzuri na wa kudumu kwa desturi za Kimashariki."

Rasilimali kuu iliyoletwa na wahamiaji wa Kiislamu huko Magharibi si nguvu zao za Kibinadamu ispokuwa ni Uislamu, ambao kwa sasa unaota mizizi hapa. Misikiti mingi na vituo vingi vya Kiislamu vimeshaanzishwa na Watu wengi wamesharejea katika Uislamu. Napendelea neno “kurejea” na sio “kubadili dini”, kwa kuwa, kila mtu anazaliwa akiwa amejisalimisha kwa Allah (Mwislamu) na kwa hiyo, kuwa Mwislamu ni maumbile ya kila mmoja. Wazazi au jamii inambadilisha kumfanya awe Myahudi, Mkristo, Imani nyinginezo, au Kukufuru.

Hili vilevile, linathibitisha kuwa Uislamu hauenei kwa upanga lakini kwa wapesi unaenea kwa kutangazwa na Mwislamu mmoja mmoja au kwa makundi. Hatuna vikundi vya misheni maalumu kama walivyonavyo Wakristo.

Idadi ya watu ulimwenguni imeongezeka kwa 136% kuanzia 1934 hadi 1984, Ukristo umeongezeka kwa 47% na Uislamu kwa 235%. Takwimu hizi unazipata katika The Plain Truth, Februari 1984, katika toleo lake la kutimiza miaka 50, zimenukuliwa kutoka The World Alamanac and Book of Facts 1935, and Reader`s Digest Alamanac and Year book 1983.

C. Ikiwa dini tatu zote, Uyahudi, Ukristo na Uislamu, zinadai zinatokana kwa Mungu Mmoja na Muumba huyo huyo, kwa nini zitofautiane?

M. Mitume yote, tangu Adamu hadi Muhammad (SAW) waliletwa wakiwa na ujumbe huo huo: utiifu kikamilifu wa binadamu kwa Allah. utiifu huu kwa Kiarabu unaitwa “Islamu,” pia unamaanisha, amani kati ya Muumba na na viumbe vyake. Kinyume na majina Uyahudi na Ukristo, jina hili Uislamu limetolewa na Allah, Mwenyewe, kama ilivyotajwa katika Qurani Sura 5:3 **"...Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na kukutimizieni neema Yangu, na Nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu....."** Si “Uyahudi” wala “Ukristo” unaopatikana katika Biblia au kamusi ya Biblia. Hakuna Nabii wa Kiisraeli aliyesema neno

[4] Eneo la nchi ya Saudia, na maeneo yaliyo karibu na Saudia.

"Uyahudi." Yesu kamwe hajadai kuuanzisha Ukristo na kamwe hajajiita Mkristo. Neno "Ukristo" limetajwa mara tatu tu katika Agano Jipya mara ya kwanza lilitumiwa na Wapagani na Wayahudi wa Antokia, mnamo mwaka 43 AD., muda mrefu baada ya kuondoka kwa Yesu na kuiacha dunia hii." Soma katika Matendo 11:26 **"... Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antokia."** Baadaye, litumiwa na mfalme Agripa wa pili kamweleza Paulo katika Matendo 26:28 "**Agripa akamwambia Paulo, Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo."**

Kwa hiyo jina Ukristo, kwanza kabisa lilitolewa na maadui wa Ukristo si marafiki. Na hatimaye lilitumiwa na Petro katika waraka wake wa kumfariji mwenye imani, katika 1 Petro 4:16 **"Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya..."**

Mwislamu wa kwanza duniani si Muhammad (SAW), bali ni Ibrahimu, aliyejisalimisha kikamilifu kwa Allah. Likini Uislamu ukiwa ni njia ya maisha umefunuliwa kwa Mitume mingine iliyomtangulia Ibrahimu, kama vile Adamu na Nuhu. Kwa hiyo, Uislamu ndiyo njia ya maisha ya wanadamu wote.

C. Vipi Ibrahimu atakuwa Mwislamu? Wakati inajulikana kuwa yeye ni Myahudi.

M. Myahudi? Nani aliyekwambia hilo?

C. Tumefundishwa hivyo, kwa hiyo hilo lazima linathibitishwa na Biblia.

M. Je, unaweza kunionyesha ni wapi katika Biblia panaposema kuwa yeye alikuwa ni Myahudi? Kama huwezi kupapata kirahisi, acha nikusaidie. Soma Mwanzo 11:31

C. **"Tera akamtwaa Abramu mwanawe, na Lutu mwana wa Harani, mwana wa mwanawe, na Sarai mkwewe, mke wa Abramu mwanawe, wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani, wakafika mpaka Harani wakakaa huko."**

M. Kwa hiyo, Ibrahimu alizaliwa Uru wa Wakaldayo na hawezi kuwa Myahudi. Kwanza kwa sababu Uru wa Wakaldayo ilikuwa Mesopotamia, ambako kwa sasa ni sehemu ya Iraq. Kwa hiyo, Yeye alikuwa ni Mwarabu zaidi kuliko Myahudi. Pili neno "Uyahudi" limekuja baada ya kuishi kwa Yudah, mjukuu mkubwa wa Ibrahimu. Soma zaidi, Mwanzo 12:4-5

C. **"... Naye Abramu alikuwa ni mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani... nao wakaingia katika nchi ya Kanaani."**

M. Kwa hiyo Ibrahimu alihamia Kanaani akiwa na miaka sabini na mitano na Biblia kwa uwazi inataja kuwa, Ibrahimu alikuwa huko akiwa ni mgeni. Mwanzo 17:8 **"Nami nitakupa wewe na uzao wako baada yako nchi hii unayoikaa ugeni, nchi yote ya Kanaani, kuwa milki ya milele, nami nitakuwa Mungu wao."** Sasa soma Mwanzo 14:13.

C. **“Mtu mmoja aliyeponyoka akaenda, akampasha habari Abramu Mwebrania;...”**

M. Vipi unamwita Ibrahimu Myahudi kama Biblia yenyewe inamwita Mwebrania jina ambalo maana yake ni mtu kutokea upande mwingine wa mto Euphrates. Pia linamaanisha kufungamana na Eber, mjukuu wa Shem. Sasa soma katika Mwanzo 32:28 kile kilichotokea kwa jina Yakobo baada ya mieleka na Malaika.

C. **"Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe ukashinda."**

M. Kwa hiyo Ibrahimu alikuwa ni Mwebrania. Na wajukuu wa yakobo walikuwa ni Waisraeli yakiwemo makabila kumi na mawili. Yuda alipewa jina la utani la "Yahudi" kwa hiyo, wajukuu wa Yuda peke yao ndiyo waliokuwa Wayahudi kwa asili. Na ili kumjua ni nani hasa ndiyo alikuwa Musa, soma Kutoka 6:16-20.

C. **"Na haya ndiyo majina ya wana wa Lawi, sawasawa na vizazi vyao; Gershoni, na Kohath, na Merari; na miaka ya maisha yake Lawi ilikuwa ni miaka mia na thelathini na saba. Wana wa Gershoni; ni Lbni, na Shimei, sawasawa na jamaa zao. Na wana wa kohathi; ni Amramu, na Ishari, na Hebroni, na Uzieli; na miaka ya maisha ya huyo Kohathi ilikuwa ni miaka mia na thelathini na mitatu. Na wana wa Merari; ni Mali, na Mushi. Hizi ni jamaa za hao Walawi sawasawa na vizazi vyao. Huyo Amramu akamwona Yokebedi ndugu ya baba yake; naye akamzalia Haruni, na Musa..."**

M. Kwa hiyo, Musa hakuwa Myahudi kwa sababu hakuwa mjukuu wa Yuda lakini ni wa Lawi. Musa alipewa Torati (sheria) kwa wana wa Israeli.

C. Unalifasiri vipi jambo hilo?

M. Kwa kuwa sisi tunatumia Qurani kama ni kipimo. Unaweza kuifafanua Biblia na kusahihisha maoni ya Kiyahudi na Kikristo kwa Muktadha wa Qurani. Qurani ni kitabu kilichofunuliwa mwisho, hakijaharibiwa wala kughushiwa. Yaliyo ndani yake Allah ameyadhamini, katika Sura 2:2: **"Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake;....."** pia katika Sura ya 15:9 **"Hakika Sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Qurani); na hakika Sisi ndio tutakayoyalinda."** Aya hii ni changamoto kwa wanadamu. Ni ukweli wa wazi kuwa zaidi ya miaka elfu moja na mia nne imeshapita hakuna hata herufi moja ya Qurani hii iliyobadilishwa ingawa makafiri wamejaribu kwa kila liwezekanalo kuibadilisha, lakini wameshindwa kwa unyonge katika juhudi zao hizo. Kama ilivyotajwa katika aya hii tukufu: **"Hakika Sisi ndio tutakayoyalinda" na Allah, ameshailinda.**

Kinyume chake, vitabu vitakatifu vingine vyote (Torati, Zaburi, Injili, nk) vimeshaghushiwa kwa njia ya kuongeza, kufuta au kubadilisha asili yake.

C. Qurani inasema nini juu ya Ibrahimu na Musa linalothibitishwa na Biblia?

M. Katika Sura 3:65: **"Enyi watu mliopewa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahimu, na hali Taurati na Injili havikuteremshwa ila baada yake? Basi je, hamfahamu?"** Na katika Sura 3:67: **"Ibrahimu hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii; wala hakuwa katika washirikina."** Katika Sura 2:140: "**Mnasema (nyinyi Mayahudi na Manasara) kuwa Ibrahimu na Ismaili na Is-haqa na Yaaqubu na kizazi (chake) walikuwa Mayahudi (kama nyinyi)? Sema: "Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nina dhalimu mkubwa kuliko yule afichae ushahidi alionao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na hayo mnayoyafanya."**

C. Ni ajabu kusikia jina Allah. Kwa nini husemi "God" ukiwa unaongea Kingerza?

M. Naam, bila shaka, jina "Allah" linaonekana ni geni kwa wasiokuwa Waislamu, lakini jina hili limeshatumiwa na Mitume yote tangu Adamu mpaka Muhammad (AS). Nalo ni ufupisho wa maneno mawili ya Kiarabu; Al – Ilah, yaani Mwenyezi Mungu. Kwa kuiondosha herufi "I" utapata neno Allah. Kwa mujibu wa nafasi yake katika tungo (sentesi) ya Kiarabu jina hilo linaweza kuwa na umbo la "Allaha" ambalo ni karibu na jina la Muumba kwa Kiebrania yaani "Eloha." Lakini Wayahudi wanatumia kimakosa umbo la wingi "Elohim," linaloashiria zaidi ya Mungu Mmoja. Neno "Allaha" lina matamshi yanayokaribiana na neno la

Kiarama linalojulisha Mungu lugha iliyotumiwa na Yesu, kwa kulitaja "Alaha" (Tazama Insaiklopidia Britannica 1980 chini ya neno “Allah” na “Elohim”). Kwa hiyo, wakati jina “Allah” ni geni kwa wasio Waislamu, lakini si geni kwa Mitume yote tangu Adamu mpaka Muhammad, (AS) kama walivyotangaza misingi ile ile ya Uislamu (utiifu kamilifu) na neno “Allah” linamaanisha jina la Mungu Aliye Hai. Jina hilo halina wingi au ujinsia, kwa hiyo hakuna kitu kama “Allahs-Miungu,” au “Allah,” wa kiume au wa kike, kama ilivyo, katika lugha ya Kingereza yenye miungu ya kiume na kike (Gods or Goddess). Pia ni jambo la kuchanganya kutumia neno God, kwa vile Wakristo wengi wanaozungumza Kingereza wanamzingatia Yesu kuwa ni Mungu. Hata neno “Muumba” pia linachanganya, kwa kuwa Wakristo wanashikilia kuwa Yesu ameumba dunia. Si tu jina “Allah”, ndilo geni, lakini pia njia wanazozitumia Waislamu kumwabudu Allah wakiwa na udhu, unyenyekevu, kurukuu, kusujudu na kufunga, nazo ni ngeni kwa wasio Waislamu, lakini si ngeni kwa mitume yote. Wakati udhu (kuosha uso, mikono, miguu, na kupaka maji kicwani), kabla ya kusali, haufanywi na Wakristo wa leo lakini jambo hilo lilifanywa na Waislamu na mitume iliyotangulia, kama inavyoonekana katika vifungu vya Biblia vifuatavyo: Kutoka 40:31-32 **"Musa na Haruni, na wanawe wakanawa mikono yao na miguu yao ndani yake; hapo walipoingia hema ya kukutania, na hapo walipoikaribia madhabahu, walinawa kama BWANA alivyomwamuru Musa"**. Ingawa Paulo amefanya mabadiliko mengi katika mafundisho ya Yesu (AS), lakini alikuwa mwaminifu katika kuuheshimu udhu, kama inavyoonekana katika Matendo 21:26. **"Ndipo Paulo akawatwaa wanaume wale, na siku ya pili yake akajitakasa nafsi yake pamoja nao, akaingia ndani ya hekalu...."** Na 1 Wakorinto 11:5-6, 13: **"Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu, bila kufunika kichwa, yuaibisha kichwa chake; kwa maana ni sawasawa na yule aliyenyolewa. Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele. Au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au konyolewa, na afunikwe."** Wanawake wa Kiislamu wanatekeleza swala zao huku wamefunika vichwa vyao. Amua wewe mwenyewe; Je, ni vizuri kwa mwanamke aswali mbele ya Mungu huku kichwa chake kimefunikwa au hakijafunikwa? Waislamu wanaabudu kwa unyenyekevu, kurukuu, kusujudu na bila ya viatu kama ilivyofanywa na Mitume iliyotanguli. Zaburi 95:6 **"Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba.**” Yoshua 5:14 **"Akasema, La, lakini nimekuja sasa, nili amiri wa jeshi la BWANA. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu aniambia nini mimi mtumishi wake?"** 1 Wafalme 18:42 **"Basi Ahabu akainuka ili ale na kunywa, Naye Eliya akapanda juu mpaka kilele cha Karmeli; akasujudu kifudifudi, akainama uso mpaka**

**magotini."** Hesabu 20:6 **"Musa na Haruni wakatoka pale palipokuwa mkutano, wakaenda hata mlangoni pa hema ya kukutania, wakaanguka kifudifudi; utukufu wa BWANA ukawatokea."** Mwanzo 17: 3 **"Abramu akaanguka kifudifudi Mungu akamwambia akasema."** Kutoka 3:5 **"Naye akasema, Usikarabie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu."** Na Matendo 7:33 **"Bwana akamwambia, vua viatu miguuni mwako, kwa maana mahali hapa unaposimama ni nchi takatifu."**[5]

Wakristo watapatwa na mshtuko wakisikia kuwa Hija, inayojumuisha tukio la Waislamu kuizunguka jiwe tukufu (yaani Kaaba)[6], huko Maka, imeshafanywa na Mitume wengi, hata na Mitume ya Kiisraeli.

C. Kamwe sijasoma kitu Hija au Jiwe takatifu (yaani Kaaba) ndani ya Biblia.

M. Hilo limetajwa wazi wazi kwa mara nyingi lakini kikawaida linatazamwa kijuu juu na wasomaji wa Biblia. Kwa mfano:

1. **"Yakobo alipokuwa nijani kuelekea Padaram aliona maono na akajenga nguzo ya jiwe usiku, asubuhi iliyofuatia, aliyoiita Beth – El, yaani Nyumba ya Bwana.¨** Mwanzo 28:18 -19
2. Miaka mingi baadaye Mtume huyo huyo, Yakobo, aliamrishwa na Allah aende Beth-El (Mwanzo 35:4-5). Yakobo aliondosha miungu yote ya uongo na ya kisanamu na akaondoa masanamu yote kabla ya kwenda huko. Karne nyingi baadaye Mtume Muhammad (SAW) naye aliharibu masanamu yote 360 yaliyokuwa yanazunguka jiwe takatifu (Kaaba) huko Maka.
3. Nguzo nyingine ilijengwa na Yakobo pamoja na baba mkwe wake, Laban, (Mwanzo 31:45-49) **"Yakobo akatwaa jiwe akalisimamisha kama nguzo. Yakobo akawaambia ndugu zake, kusanyeni mawe. Wakatwaa mawe wakafanya chungu, nao wakala huko karibu na ile chungu. Labani aliita Yegarsahadutha, lakini Yakobo aliiita Galedi. Labani akasema chungu hii ni shahidi kati ya mimi na wewe hivi leo. Kwa hiyo likaitwa jina lake Galedi, na Mispa, maana alisema Mungu avizie kati ya mimi na wewe, wakati tusipoonana."**
4. Jephthah na Ammon walipigana vita. Jephthah aliapa kwa BWANA katika Mispa ya Galedi kuwa atamtoa sadaka binti yake wa pekee kama angeshinda. Kwa hakika alishinda, na akamchoma

[5] Kusali na viatu visafi kunaruhusiwa na suna, lakini msikitini hairuhusiwi kuingia na viatu.
[6] Jiwe jeusi huko Maka

binti yake akiwa hai katika eneo hilo ikiwa ni sadaka kwa BWANA. Waamuzi 11:29-39.

5. Askari wa mapanga laki nne wa makabila kumi na moja ya Israeli waliapa mbele za Bwana katika Mispa waliangamize kabila la Benjamini. (Waamuzi 20 na 21).
6. Wana wa Israeli, chini ya Samweli, waliapa katika Mispa kuangamiza masanamu yao kama watashinda dhidi ya Wafilisti (1 Samweli 7).
7. Taifa zima la Israeli lilijikusanya katika Mispa wakati Samweli aliposimikwa ufalme wa Israeli (1 Samweli 10).

Ni wazi kwa sasa, kuwa hakuna Mispa iliyobakia ulimwenguni, ispokuwa ile kongwe kabisa iliyopo katika Mji Mtakatifu wa Maka iliyojengwa na Ibrahimu na mwanawe Ismaili, na kutokana naye, Mtume Muhammad aliibuka hapo baadaye. Waislamu ni wafuasi wa kweli wa Mitume yote. Naweza kukueleza vitu vingine kuhusu Waislamu, Uislamu na Muhammad (SAW) katika Biblia, lakini tunaweza kujadili zaidi ikiwa kama ni kweli unatafuta ukweli kwa bidii tu.

C. Nina hakika na imani yangu kama Mkristo lakini pia nimehamasika kujua mengi ya ziada kuhusu dini zote mbili. Mara nyingine nahisi fedheha nikiwa ni Mkristo baada ya kusoma vitabu vilivyoandikwa na Waislamu.

M. Je hilo linakuathiri katika maisha yako ya kidini?

C. Ndiyo. Siendi kanisani kama kawaida ya zamani. Na nimekuwa ninasoma vitabu vilivyoandikwa na Waislamu. Nimeshawauliza Waislamu wengi wafafanue mambo yaliyokuwa hayapo wazi kwangu, lakini sijakinaika. Natafuta imani nitakayoitumainia, na kunipa amani moyoni, inayokubalika kisayansi, na ile nisiyolazimika kuiamini kibubusa (kiupofu).

M. Naheshimu mawazo yako. Hata hivyo, kwa kuwa haturuhusiwi kulazimisha watu kuwa Waislamu, nataka kuhakikisha kuwa, kwa hakika umeshavutiwa na kujifunza ukweli, kabla sijaendelea.

C. Unakusudia kuwa ninaweza kuamini kile nitakacho na kuwa hakuna mtu awezaye kunilazimisha kitu kingine?

M. Ndiyo, kwa vile Qurani inasema kuwa hakuna kulazimishana kuingia katika dini.

C. Sasa, Kwa nini Waislamu wanawaita watu waukubali Uislamu?

M. Kama Wakristo wanavyowataka Wayahudi wamkubali Yesu kuwa ni Masihi, nasi Waislamu tunawataka Wakristo, vile vile Wayahudi na watu wote, wamkubali Muhammad (SAW) kuwa ni Mtume wa mwisho. Mtume wetu Muhammad (SAW) amesema: **"Fikisheni ujumbe wangu hata kama ni aya moja."** (Aya ya Qurani Takatifu).

Pia, yametajwa katika Isaya 21:13, **"Ufunuo juu ya Arabuni. Ndani ya mwitu wa Arabuni mtalala, Enyi misafara ya Wadedani."** Ambayo inamaanisha majukumu ya Waislamu wa Kiarabu ya kueneza mafundisho ya Uislamu. Isaya ameonyesha hayo baada ya kuona katika maono kundi la  wapanda punda na kundi la wapanda ngamia. Isaya 21:7 **"Naye akiona kundi la wapanda farasi, wakienda wawili wawili, na kundi la punda, na kundi la ngamia; asikilize sana, akajitahidi kusikiliza."**

Kunndi la punda limebadilika na kuwa la Yesu (AS), aliyeingia Jerusalemu. Yohana 12:14; Matayo 21:5. Nani mwenye kundi la ngamia? Atakuwa nani mwingine zaidi ya Muhammad (SAW), aliyekuja takriban miaka mia sita baada ya kuja kwa Yesu (AS). Kama hili halikubaliki, kwa hiyo uatabiri huu haujatimia.

C. Ufafanuzi wako unanihamasisha niisome Biblia kwa uangalifu zaidi. Ningependa niwe na mazungumzo mengi na wewe.

M. Ndiyo, kama umefanikiwa hapa duniani, hiyo haimaanishi kuwa utafanikiwa na huko Ahera. Ahera ni bora zaidi na ni yenye kudumu kuliko maisha haya. Watu kwa sasa, wanazidi kuwa wapenda mali na maisha ya yasiyo ya kidini. Hebu tujumuike mara kwa mara ili tuzungumzie tofauti zilizopo kwa uwazi bila upendeleo. Uislamu umejengeka kwa hoja, na hutakiwi kuukubali hivi hivi tu! Hata Biblia yako inasema: **“Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema.”** 1 Wathesalonike 5:21.

C. Sasa hivi umetaja “wapanda ngamia” kutoka katika Isaya na ukahitimisha kuwa huyo alikuwa ni Muhammad. Je, huyo Muhammad ametabiriwa katika Biblia?

M. Bila shaka.

C. Katika Agano la Kale au Jipya?

M. Katika yote mawili. Lakini wewe huwezi kumtambua huyo Muhammad ndani ya Biblia kwa kuwa bado unaendelea kutoamini

Mungu Mmoja, bado unaendelea kuamini Utatu, Uungu wa Yesu, Yesu Mtoto wa Mungu, Dhambi ya asili na Mateso ya Yesu kama ndiyo uwokovu. Yote haya yalifanywa na wanadamu. Yesu ametabiri kuwa, watu watamwabudu yeye bila maana na wataamini imani zilizoundwa na wanadamu: **"Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu."** (Matayo 15:9).

## Biblia Takatifu

M. Je, una uhakika kuwa Biblia ni neno Takatifu?

C. Ndiyo, nina hakika sana kuhusu hilo, hilo ni neno la Mungu.

M. Soma alichokisema Luka kuhusu uandishi wake katika Luka 1:2-3.

C. **"....Kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo mtukufu."**

M. Kama Luka amesema kuwa yeye mwenyewe hakuwa shahidi aliyeshuhudia kwa macho yake na maelezo aliyoyakusanya yalitokana na mashahidi walioshuhudia kwa macho na sio kama maneno yaliyofunuliwa na Mungu, Je utaendelea kuamini kuwa Biblia ni Neno la Mungu?

C. Huenda ni kifungu hiki tu, ndicho kisicho Neno la Mungu.

M. Historia imeonyesha kuwa Biblia imeshabadilishwa. The Revised Standard Version (1952 na 1971), Biblia ya The New American Standard Bible na The New World Translation zimefuta mistari (aya) maalumu zinazopatikana katika King James Version. Reader`s Digest imeshapunguza Agano la Kale kwa asilimia hamsini 50 na Agano Jipya kwa asilimia ishirini na tano 25. Miaka kadhaa iliyopita wanatiolojia wa Kikristo walitaka "kui-desex" (kuondosha viungo vya uzazi/ujinsia) Biblia. Je, neno "takatifu" linamaanisha kuwa Biblia haina makosa?

C. Ndiyo hivyo. Lakini unakusudia kosa la aina gani?

M. Chukulia kuwa aya moja inaeleza kuwa mtu fulani amekufa akiwa na miaka hamsini na aya nyingine inaeleza kuwa mtu huyo huyo amekufa akiwa na miaka sitini. Je, maelezo yote mawali ni sahihi?

C. Hapana, ni moja tu itakayokuwa sahihi au zote zitakuwa za uwongo.

M. Kama kitabu kitakatifu kina aya zinazopingana, je, utaendelea kukitambua kuwa ni kitakatifu?

C. Bila shaka hapana, kwa kuwa maandiko matakatifu ni ufunuo utokao kwa Mungu. Kwa hiyo, haiwezekani kwa makosa au aya zinazopingana. Kuwemo ndani yake.

M. Kwa hiyo, Biblia si takatifu.

C. Sawa! Kwa hali hiyo, utakatifu wake unatoweka.

M. Kama ni hivyo, huwezi kuiamini kwa asilimia mia moja. Nini sababu ya makosa hayo?

C. Huenda ni makosa ya unukuzi au mabadiliko ya makusudi ya waledi, kama vile kufuta au kuongeza ndani ya Biblia.

M. Kama kuna aya zinazogongana ndani ya Biblia, je, utaendelea kuizingatia Biblia kuwa ni takatifu?

C. Naamini Biblia ni takatifu, kwa kuwa sijaona aya zinazopingana.

M. Kuna aya nyingi zinazopingana ndani yake.

C. Katika Agano la Kale au Jipya?

M. Katika maagano yote mawili. Hizi ni baadhi ya aya hizo:

2 Samweli 8:4

**Daudi akampokonya wapanda farasi elfu na mia saba, na askari waliokwenda kwa miguu ishirini elfu...**

1 Nyakati 18:4

**Daudi akampokonya magari elfu, na wapanda farasi saba elfu, na askari waendao kwa miguu ishirini elfu...**

Swali; Mia saba au saba elfu?

II Samweli 8:9-10

**Na Tou, (When Toi) mfalme wa Hamathi, aliposikia ya kwamba Daudi amewapiga jeshi lote la Hadadezeri, Tou (Toi) akamtuma kwa Daudi Hadoramu (Joramu) mwanawe kusalimia, na kumbarikia, kwa sababu amepigana na Hadadezeri, na kumpiga; kwa maana Hadadezeri alikuwa amepigana vita juu ya Tou (Toi). Na mkononi mwake akaleta vyombo vya fedha, na vyombo vya dhahabu, na vyombo vya shaba.**[7]

[7] Hapa unaona matatizo ya wafasiri, Mwandishi wa kitabu alikuwa anatumia Biblia ya Kingereza ambayo imeyaandika hayo majina kwa herufi tofauti, ndio akajenga hoja yake, lakini ajabu tafsiri

1 Nyakati 18:9-10

**Hata aliposikia Tou, (Tou) mfalme wa Hamathi, na kuwa Daudi amewapiga jeshi lote la Hadadezeri (Hadarezer), mfalme wa Soba, Daudi akampeleka mwanawe Hadoramu kwa mfalme Daudi, ili kumsalimia, na kumbariki, kwa sababu alikuwa amepigana Hadadezeri (Hadarezer), na kumpiga; kwa maana Hadadezeri (Hadarezer) alikuwa amepigana vita juu ya Tou; naye akaleta vyombo vya dhahabu, na fedha, na shaba, vya namna zote.**

Swali: Ni Toi au Tou? Joram au Hadoramu? Hadadezer au Hadarezer?

2 Samweli 10:18

**Wakakimbia Washami mbele ya Israeli; naye Daudi akawaua katika Washami, watu wa magari mia saba, na wapanda farasi arobaini elfu, naye akampiga huyo Shobaki, jemadari wa jeshi lao, hata akafa huko.**

1 Nyakati 19:18

**Washami wakakimbia mbele ya Israeli; naye Daudi akawaua katika Washami, watu wa magari saba elfu, na askari waendao kwa miguu arobaini elfu na akamwua na Shobaki, jemadari wa jeshi.**

Swali: Watu wa magari mia saba au waendao kwa miguu elfu saba? wapanda farasi arobaini elfu au waenda kwa miguu? Shobach au Shophach?[8]

2 wafalme 8:26

**Ahazia alikuwa na umri wa miaka ishirini na miwili alipoanza kutawala...**

2 Nyakati 22:2

**Ahazia alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili alipoanza kutawala...**

---

Biblia ninayoitumia "SWAHILI UNION BIBLE (1952 edition) UBS 35M 2007", imeyafanya majina hayo yawe na herufi zinazofana hadi zinaharibu hoja ya mtunzi kama si ufafanuzi huu. Kwa hakika hoja yake ni ya msingi kwa wanaotumia Kingereza na kama wafasiri wa Biblia wa Kiswahili wangezingatia kuandika Majina kama yalivyo!!

[8] Tatizo la majina ni la Biblia ya kiswahili Ukitazama ya Kingereza utaona tofauti za majina hayo!! Kama nilivyoeleza katika footnote namba saba!

Swali: miaka ishirini na miwili au arobaini na miwili?

2 Wafalme 24:8

**Yekonia alikuwa na umri wa miaka kumi na minane alipoanza kutawala; akatawala miezi mitatu katika Yerusalemu...**

2 Nyakati 36:9

**Yekonia alikuwa na umri wa miaka kumi na minane** *(hii kumi na nane ipo hapa katika Biblia ya Kiswahili, lakini katika Kings James Verson imeandikwa maika minane!!)* **alipoanza kutawala; akatawala katika Yerusalemu miezi mitatu na siku kumi."**

**Swali: Miaka kumi na minane au minane? Miezi mitatu au miezi mitatu na siku kumi?**

2 Samweli 23:8

**Haya ndiyo majina ya mashujaa alokuwa nao Daudi; Yashobeamu** (Tachmonite - kwa Kingereza)**, Mhakmoni, mkuu wa maakida; huyu aliliinua shoka lake juu ya watu mia nane waliouawa pamoja.**

1 Nyakati 11:11

**Na hii ndiyo hesabu ya hao mashujaa alokuwa nao Daudi; Yashobeamu** (Jashobeam – kwa Kingereza)**, Mhakmoni, mkuu wa maakida; huyo aliuinua mkuki wake juu ya watu mia tatu, akawaua pamoja.**

Swali: Tachmonite au Hachmonite? Watu mia nane au mia tatu?

2 Samweli 24:1

**Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akasema, Nenda ukawahesabu Israeli na Yuda.**

1 Nyakati 21:1

**Tena Shetani akasimama juu ya Israeli, akamshawishi Daudi, kuwahesabu Israeli.**

Swali: Je, Shetani ndiye Bwana wa Daudi? Mungu aepushe hilo!

2 Samweli 6:23

**Basi** (Mikali = Michal kwa Kingereza)**, binti Sauli, hakuwa na mtoto hata siku ya kufa kwake.**

2 Samweli 21:8

**Ila Mfalme akawatwaa hao wana wawili wa Rispa, binti Aya, aliomzalia Sauli, Armoni na Mefiboshethi; na wana watano wa** (Merabu = Michal kwa Kingereza) **binti Sauli, aliomzalia Adrieli, mwana wa Barzilai, Mmeholath.**

Swali: Je, Mikali alikuwa na watoto au hakuwa na watoto? Zingatia: Hilo jina Mikal katika 2 Samweli 21:8 bado lipo ndani ya Biblia ya The King James Version and The New World Translation of the Holy Scriptures inayotumika na Mashahidi wa Yehova, lakini limeshabadilishwa na kuwa Merabu katika The New American Standard Bible (1973).

C. Sijapatapo kuona chochote katika hayo hapo kabla. Je, kuna ziada?

M. Je, bado unataka kusikia ziada? Je, mifano hii haitoshi kuweza kuukana utakatifu wa Biblia? Tazama Mwanzo 6:3 **"BWANA akasema, roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini."**

Sasa, Nuhu alikuwa na miaka mingapi alipokufa? Zaidi ya miaka mia na ishirini. Tazama Mwanzo 9:29 **"Siku zote za Nuhu zilikuwa miaka mia kenda na hamsini, akafa."** Baadhi ya wanatiolojia wa Kikristo wanadai kuwa hili halimaanishi kuwa kiwango cha juu zaidi cha uhai wa mwanadamu kitakuwa ni miaka mia na ishirini, lakini inamaanisha kuwa mafuriko ya Nuhu ndiyo yangetokea katika mwaka wa mia na ishirini. Hata maelezo haya hayatoshi, kwa kuwa wakati wa mafuriko Nuhu angekuwa na umri wa miaka mia sita na ishirini (500 + 120). Hata hivyo, Biblia inaeleza kuwa Nuhu alikuwa na miaka mia sita. Soma Mwanzo 5:32 **"Nuhu alikuwa mwenye miaka mia tano..."** Mwanzo 7:6 **"Naye Nuhu alikuwa mtu wa miaka mia sita hapo hiyo gharika ya maji ilipokuwa juu ya nchi."**

Wakristo wanaamini kuwa Mungu amemuumba binadamu kwa mfano Wake: mweupe, mweusi, au rangi yoyote, mwanamume aua mwanamke? Haya ni kwa mujibu wa Mwanzo 1:26 **"Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa Sura yetu;..."** Lakini hili linapingana na Isaya 40:18, 25: **"Basi mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani?..." "Mtanifananisha na nani, basi nipate kuwa sawa naye? Asema yeye aliye Mtakatifu."** Pia tazama Zaburi 89:6 "**Maana ni nani katika mbingu awezaye**

**kulinganishwa na BWANA? Ni nani afananaye na BWANA miongoni mwa mwalaika?**” Na Yeremia 10:6,7 **"Hapana hata mmoja aliye kama wewe, Ee BWANA;..." "... hapana hata mmoja kama wewe."**

C. Lakini yote hayo yapo katika Agano la Kale.

M. Vizuri, hebu twende katika Agano Jipya.

Yohana 5:37 **"Naye Baba aliyenipeleka amenishuhudia. Sauti yake hamkuisikia wakati wo wote, wala sura yake hamkuiona.”**

Yohana 14:9 **".... Aliyeniona mimi amemwona Baba... "** .

Yohana 5:31 **"...mimi Nikijishuhudia mwenyewe, ushahidi wangu hauwezi kukubaliwa kuwa wa kweli.''**

Yohana 8:14 **"Yesu akajibu, akawaambia Mimi ningawa ninajishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu ndio kweli..."**

Hii ni mifano michache tu ya migongano ndani ya Agano Jipya. Utapata migongano zaidi kama tutazungumzia ukweli wa imani za Wakristo wa kisasa kama vile imani ya Utatu, Uungu wa Yesu Kristo, Mtoto wa Mungu kwa Yesu, Dhambi ya Asili na Mateso Msalabani ndio uwokovu, bila kutaja namna Biblia ilivyowashushia hadhi manabii, kuwa waliabudu miungu ya uwongo, kuingiliana ndugu kwa ndugu, kubaka, na uzinzi.

C. Wapi unapoyapata hayo katika Biblia?

M. Nuhu anaripotiwa kuwa alilewa hadi akawa uchi mbele ya watoto wake walio wakubwa (Mwanzo 9:23-24): **"Shemu na Yafethi wakatwaa vazi, wakalitanda mabegani mwao wote wawili, wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao; na nyuso zao zilielekea nyuma, wala hawakuuona uchi wa baba yao. Nuhu akaelevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea.”**

Suleimani ameshutumiwa si kwa kuwa ana vimada vingi sana, lakini pia kuabudu miungu ya uwongo (1 Wafalme 11:9-10) **"Basi BWANA akamghadhibikia Sulemani kwa sababu moyo wake umegeuka, naye amemwacha BWANA, Mungu wa Israeli, aliyemtokea mara mbili, akamwamuru katika habari ya jambo hilo hilo asifuate miungu mingine; lakini yeye hakuyashika aliyoyaamuru BWANA."**

Haruna, mtume aliyeongozana na Musa, nduguye, katika kazi yake kwa Firauni, alituhumiwa kuwa amewaundia wana wa Israeli ndama wa dhahabu ili wamwabudu (Kutoka 32:4): **"Akaipokea mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha; nao wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli iliyokutoa katika nchi ya Misri."**

Unaweza kusoma juu ya Lutu anakabiliwa na tuhuma za kujamiiana kwa maharimu na mabinti zake wawili (Mwanzo 19:36): **"Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao"**

Unaweza kusoma juu ya mtume aliyeoa wanawake wawili ambao ni ndugu kwa wakati mmoja (Mwanzo 29:28): **"Yakobo akafanya hivi, akatimiza siku saba, Naye akampa Raheli bibti yake kuwa mkewe."**

Na mtume mwingine ametuhumiwa kwa uzinzi (2 samweli 11:4-5): **"Basi Daudi akapeleka wajumbe, akamtwaa; {mke wa Uriiah} naye akaingia kwake; naye akalala naye; (maana yule mwanamke amekwisha kutakasika unajisi wake); kisha akarudi nyumbani kwake. Yule mwanamke akachukua mimba; basi akapeleka na kumwambia Daudi, akasema, Ni mja mzito"**

Swali langu: Vipi Daudi anakubaliwa kuwa ni katika kizazi cha Yesu wakati ameelezwa ni mtu aliyefanya uzinzi? Allah aepushie mbali jambo hilo! Je, hili halipingani na kile kilichotajwa katika Kumbukumbu la Torati 23:2 **"Mwana wa haramu asiingie katika mkutano wa BWANA; hata kizazi cha kumi asiingie aliye wake katika mkutano wa BWANA."**

Tuhuma nyingine ni kuingiliana ndugu na kubaka dhidi ya Ammon, mtoto wa Daudi, na dada yake wa kambo Tamar (2 Samweli 13:14): **"Walakini yeye hakukubali kusikiliza sauti yake; naye akiwa na nguvu kuliko yeye, akamtenza nguvu, akalala naye."**

Ubakaji mwingine wenye pande nyingi unaendelea, ulifanywa na Absalom dhidi ya masuria wa Daudi, unaosimuliwa katika 2 Samweli 16:22 **"Basi wakamtandikia Absalomu hema juu ya nyumba darini; naye Absalomu akaingia kwa masuria ya babaye machoni pa Israeli wote."**

Kuingiliana ndugu kwingine, kumefanywa na Yuda na Tamari (mke wa mwanawe) Mwanzo 38:15-18 **"Yuda alipomwona alimdhania kuwa ni kahaba, maana amejifunika uso, akamgeukia kando ya njia, akasema, Niruhusu niingie kwako. Maana hakujua kuwa ni**

**mkwewe. Akamwuliza utanipa nini, ukiingia kwangu? Akasema, nitakuletea mwana-mbuzi wa kundini. Naye akamwuliza, Je! Utanipa rehani hata utakapomleta? Akasema, Nikupe rehani gani? Akamjibu, Pete yako ya muhuri, na kamba yake, na fimbo yako iliyo mkononi mwako. Basi akampa, akaingia kwake, naye akapata mimba."**

Ingawa Wayahudi na Waislamu mara nyingi wana mitazamo tofauti, lakini hakuna Mwislamu atakayediriki kuandika kitabu na kumbandika mtume yoyote wa Israeli kama vile, Yuda, Daudi, Yesu na wengineo, tuhuma za kubaka, uzinzi, kuingiliana maharimu (ndugu kwa ndugu), au umalaya. Mitume yote ilitumwa na Allah ili kuwaongoza wanadamu. Je, unadhani kuwa Mungu amepeleka watu wabaya waje kuongoza?

C. Sifikirii hivyo. Lakini je, huiamini Biblia?

M. Sisi tunaamini maandiko matakatifu yote, lakini yakiwa katika mfumo wake wa asili. Mungu ametuma mitume kwa kila taifa wakiwa ni waonyaji, na baadhi yao walikuwa na maandiko kama mwongozo kwa taifa maalumu tu. Al-Suhufu (Nyaraka) zilipelekwa kwa Ibrahimu, Torati (sehemu ya Agano la Kale) kwa Musa, Zaburi (Psalms) kwa Daudi, na Injili (Agano Jipya) kwa Yesu. Hakuna chochote katika vitabu hivi kilichobakia katika asili yake. Ikiwa ni sehemu ya mpango wa Allah, Yeye, hatimaye, alimtuma Muhammad akiwa ni mwisho wa mitume yote akiwa na Qurani ambayo ni mwongozo kwa wanadamu wote, sehemu yoyote na wakati wowote.

Yesu mwenyewe amesema kuwa ametumwa kwa watu wa Israeli tu (Matayo 15:24) **"Akajibu, Akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli."** Pia Matayo 1:21 **"Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."** Yesu pia amesema kuwa hakuja kubadilisha ila kukamilisha (Matayo 5:17-18) **"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie."**

C. Lakini katika Marko 16:15 Yesu amesema, **"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."**

M. Hilo linapingana na kile kilichotajwa hapo juu katika matayo 15:24 na Matayo 1:21. Pili, Marko 16:9-20 zimeondoshwa katika Biblia nyingi. The New American Standard Bible imekiweka kipande hiki katika

mabano na ikaweka maelezo yafuatayo: "Baadhi ya miswada ya kale mno inaondosha kuanzia aya 9 hadi 20." Biblia ya The New World Translation of the Holy Scriptures inayotumiwa na Mashahidi wa Yehova inakubali kuwa miswada maalumu ya kale inaongeza maelezo marefu au mafupi baada ya Marko 16:8 lakini baadhi ya miswada hiyo inaondosha aya hizo. Na Biblia ya The Revised Standard version inachapisha chini ya ukurasa rejeo lifuatalo: "Baadhi ya mamlaka za kale zaidi inakileta hicho kitabu cha Marko na kukifunga mwishoni mwa aya ya 8..." Hili linamaanisha kuwa ufufuo si kweli, kama ulivyoelezwa katika Marko 16:9.

C. Lakini Yesu amesema katika Matayo 28:19: "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

M. "Mataifa yote" lazima ifafanuliwe kuwa ni yale makabila kumi na mbili ya Israeli, vinginevyo itapingana na Matayo 15:25 na Matayo 1:21. Katika Biblia ya The New American Standard Bible na ya The New World Translation of the Holy Scriptures, kifungu hicho hakitafsiriwi kuwa, ni "all nations – mataifa yote" lakini kinatafsiriwa "all the nations, - yale mataifa yote," inayomaanisha yale mataifa (makabila) kumi na mbili ya Israeli. Je, unafikiri nini juu ya Biblia kwa sasa?

C. Sina hakika juu ya utakatifu wake kwa sasa.

M. Nina hakika utakinaishwa na uhalisi wa Uislamu tukishajadili tofauti zetu.

## Imani ya Utatu

M. Je, bado unaendelea kuamini Utatu?

C. Imesemwa katika Waraka wa Kwanza wa Yohana 5:8-9: **"Kwa maana wako watatu washuhudiao [mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja, Kisha wako watatu washuhudiao duniani], Roho, na maji, na damu; na watatu hawa hupatikana kwa habari moja..."**

M. Hayo yapo katika Biblia ya King James Version, lilochapishwa mwaka 1611, na kujenga ushahidi wa nguvu mno kwa imani ya Utatu. Lakini kwa sasa kifungu hiki cha "Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu: na watatu hawa ni umoja," kimeshaondoshwa katika Biblia ya Rivised Standard Version ya mwaka 1952 na 1971 na katika Biblia nyingine nyingi, kwa kuwa kilikuwa ni udanganyifu uliotiwa bila ya haki katika maandishi ya Kigiriki.

1 Yohana 5:7-8 katika The New American Standard Bible inasema: **"Na ni Roho anayeshuhudia, kwa sababu Roho ni kweli. Kwa maana wako watatu washuhudiao, Roho na maji, na damu, na watatu hao hupatikana kwa habari moja."** Pia Biblia ya The New World Translation of the Holy Scriptures inayotumiwa na Mashahidi wa Yehova, utakuta: **"Kwa maana kuna mashahidi watatu: roho, na maji, na damu, na watatu hao hupatikana kwa habari moja."** Siwezi jua kama hujui kuwa kifungu hiki muhimu mno kimeshaondoshwa, lakini nashangaa kwa nini wachungaji na wahubiri wange hawapo macho na jambo hili!

Utatu si kitu cha Biblia. Neno "Utatu" halipo katika Biblia au hata katika kamusi za Biblia. Kamwe halijafundishwa wala kutajwa na Yesu. Hakuna mzizi wala uthibitisho, ndani ya Biblia, wa kulikubali.

C. Lakini katika Matayo 28:19 badao tunakuta: **"...mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu"** Kipande hiki bado hakijaondoshwa. Je, huu si uthibitisho wa Utatu?

M. Hapana. Kama watu watatu wanakaa au wanakula pamoja, je, hilo linamaanisha kuwa wao wanaunda mtu mmoja? La! Kwani kuundwa kwa Utatu na Athanasius, shemasi wa Kimisri anayetokea Alexandria, kulikubaliwa na Baraza la Nicaea mwaka 325 AD (zaidi ya karne tatu baada ya kuondoka kwa Yesu). Hapana shaka Wapagani wa Kirumi waliachangia katika imani hii ya utatu wa mungu. Sabato ilibadilishwa na kuwa Jumapili na Desemba 25, siku ya kuzaliwa kwa mungu wao jua

Mithra, ikatangazwa kuwa ni Siku ya kuzaliwa Yesu, ingawa Biblia kwa uwazi kabisa imeyatabiri na kuyaharamisha mapambo ya miti ya Krismasi katika Yeremia 10:2-5 **"BWANA asema hivi, Msijifunze njia ya mataifa, wala msishangae kwa sababu ya ishara za mbinguni; maana mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo. Maana desturi za watu hao ni ubatili; maana mtu mmoja hukata mti mwituni, kazi ya mikono ya fundi na shoka. Huupamba kwa fedha na dhahabu; huukaza kwa misumari na nyundo, usitikisike. Mfano wao ni ni mfano wa mtende, kazi ya cherahani, hawasemi; hawana budi kuchukuliwa, kwa sababu hawawezi kwenda. Usiwaogope; kwa maana hawawezi kutenda uovu, wala hawana uwezo wa kutenda mema."** Kwa kuwa Wakristo wameenda mbali na mafundisho asilia ya Yesu, Mungu amemleta mtume Wake wa mwisho, Muhammad, afufue na kubatilisha mabadiliko yaliyofanywa na wanadamu: Kalenda ya Kirumi ya Julian imetambulishwa kuwa ni ya enzi za Kikristo; Nguruwe amehalalishwa; kutahiriwa kumeharamishwa na Paulo (Wagalatia 5:2 **"Tazama, mimi Paulo nawaambia ninyi ya kwamba, mkitahiriwa, Kristo hatawafaidia neno."**

Qurani inaonya katika Sura 5:73 **"Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: "Mwenyezi Mungu ni Mmoja katika (wale waungu) watatu; (Yeye ndiye wa tatu wao). Hali hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu Mmoja (tu peke yake). Na kama hawataacha hayo wayasemayo, kwa yakini itawakamata – wale wanaoendelea na ukafiri miongoni mwao – adhabu iumizayo."** Je, bado unaendelea kuamini Utatu, ambao haujafundishwa na Yesu?

C. Lakini Mungu na Yesu ni kitu kimoja (Yohana 14:11) "**Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu..."**

M. Soma Yohana 17:21.

C. **"Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu..."**

M. Hapa ni wazi kuwa Mungu na Yesu ni kitu kimoja, na Wanafunzi nao ni kitu kimoja ndani ya Yesu na Mungu. Kama Yesu ni Mungu kwa sababu yupo ndani ya Mungu, kwa nini wanafunzi wasiwe Miungu, wakati wao ni sawa na Yesu, aliye ndani ya Mungu? Kama Mungu, Yesu, na Roho Mtakatifu wanaunda umoja (Utatu) wakiwa pamoja na wanafunzi wataunda umoja wa Ukumi na Tano wa Mungu.

C. Lakini Yesu ni Mungu kwa mujibu wa Yohana 14:9: **"...Aliyeniona mimi amemwona Baba"**

M. Tazama kile kilichokuwepo kabla na baada ya Yohana 14:8 **"Filipo akamwambia, Bwana utuonyesha Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwepo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; Basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?"**

Yesu alimuuliza Filipo vipi nimwonyeshe Mungu kwa wanafunzi, kitu ambacho hakiwezekani. Unatakiwa umwamini Mungu kwa kuheshimu Viumbe vyake: jua, mwezi, viumbe vyote, na Yesu, aliyeumbwa na Mungu. Yeye amesema katika Yohana 4:24 **"Mungu ni Roho....."** na Yohana 5:37 **"... Sauti yake hamkuisikia wakati wowote, wala Sura yake hamkuiona."** Vipi utaweza kuona roho? Kile walichokiona kilikuwa ni Yesu, sio Mungu. Paulo amesema katika 1 Timotheo 6:16 **"Ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uwezo una yeye hata milele. Amina."** Kwa hiyo kile ukionacho si Mungu. Qurani inasema katika Sura 6:103 **"Macho hayamfikii (kumwona), bali yeye anayafikia macho (kuyaona na kuwaona hao wenye macho). Naye ni Mwenye kujua yaliyofichikana na yaliyo dhahiri."**

C. Ni vigumu kukikana kile tulichofundishwa tangu utotoni.

M. Huenda maswali yafuatayo yatakupa ufahamu mzuri juu ya Utatu: Roho Mtakatifu ni nani?

C. Roho (Spirit) Mtakatifu ni Roho (Ghost) Mtakatifu naye ni Mungu vile vile. Tumefundishwa kuwa Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu, Na Roho (Ghost) Mtakatifu ni Mungu. Haturuhusiwi kusema Miungu Mitatu, bali Mungu Mmoja.

M. Soma Matayo 1:18.

C. **“Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu."**

M. Linganisha hili na Luka 1:26-27.

C. **"Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbali ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu."**

M. Kuzaliwa kwa Yesu kimuujiza Matayo ametaja Roho Mtakatifu na Luka ametaja malaika Gabrieli. Roho Mtakatifu ni nani?

C. Hiyo ndiyo Kadhia, Roho Mtakatifu ni malaika Gabrieli.

M. Je, bado unaendelea kuamini Utatu kwa sasa?

C. Kwa hiyo, Mungu ni Mungu na Roho Mtakatifu (Spirit) au Roho (Ghost) Mtakatifu ni malaika Gabrieli, na Yesu ni ....

M. Hebu nikusaidie: Yesu ni mtume, mtoto wa Mariamu.

C. Vipi utatatua kile tukiitacho siri takatifu isiyosemeka?

M. Tunatumia Qurani kama ni kipimo cha kusahihisha mabadiliko yaliyofanywa na wanadamu katika maandiko ya ufunuo uliopita. Kama unamwamini Mungu Mmoja, na Yesu kama ni mtume, kwa nini huendi mbele zaidi kwa hatua moja na kumkubali Muhammad kuwa ni Mjumbe wa Mwisho? Kariri shahada au ushuhuda, baada yangu, kwanza kwa Kingereza na kisha kwa Kiarabu.

C. Nashuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah, Asiye na mshirika, na Muhammad ni mjumbe na mtume wake. Ashadu an la illaha illa allahu wahdahu la sharikah lahu wa ashhadu anna Muhammad abdahu wa rasulahu. Lakini vipi kuhusu babu na bibi zangu? Napenda kuwa nao. Wote walikuwa Wakristo.

M. Ibrahimu aliwaacha wazazi wake na babu/bibi zake pale ukweli (Uislamu) ulipofunuliwa kwake. Kila mtu ataulizwa juu nafsi yake. Huenda ukweli ulikuwa haujawafikia hao wazee wako kwa uwazi kama ulivyokufikia wewe. Qurani inasema katika Sura 17:15 **"Anayeongoka, basi anaongoka kwa maslaha ya nafsi yake mwenyewe, na anayepotea, basi anapotea kwa khasara (ya nafsi) yake mwenyewe. Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine. Na Sisi si wenye kuwaadhibisha (viumbe) mpaka Tuwapelekee Mtume (awafahamishe yaliyo ya haki, basi wakiyakataa ndipo wanapoangamizwa)."** Ukweli umeshakujia na ni shauri yako.

C. Je, naweza kuzikubali dini zote mbili Uislamu na Ukristo?

M. Hakuna kulazimishana kuingia dini. Unaweza kufanya kile utakacho. Lakini kama WEWE utachanganya imani zote mbili, hilo linamaanisha kuwa wewe bado hujajisalimisha kwa Allah. Wewe bado ni mtu asiyeamini, kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Sura 4:150-152

**"Hakika wale wanaomkanusha Mwenyezi Mungu na Mitume yake, na wanataka kutenga baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume Yake, kwa kusema: "Wengine tuna waamini na wengine tunawakataa," na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya (si ya Kiislamu khasa wala ya kikafiri). Hao ndio makafiri kweli. Na Tumewaandalia makafiri adhabu idhalilishayo. Na waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume Yake wala wasimfarikishe yeyote katika wao (bali wamewaamini wote), hao atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu."** Huenda ukakubaliana nami kama tutajadili mada nyinginezo.

C. Je, tunatakiwa kukariri shahada kabla ya kijifunza kikamilifu?

M. Punde tu unapofikia balehe na una uwezo wa kiakili, hapo utahesabiwa, sawa umeikakiri shahada au hujaikariri. Allah ameumba ulimwengu huu kwa lengo. Amekupa viungo vya kutofautisha kati ya haki na batili. Yeye ameshatuma mitume mingi wakiwa ni waonyaji. Tumeumbwa ili tumwabudu Yeye na kushindana wenyewe kwa wenyewe katika kufanya matendo mema hapa duniani.

Sura 3:191 **"Mola wetu! Hukuviumba hivi bure, Utukufu ni wako..."**

Sura 90:8-10 **"Je! Hatukumpa macho mawili? Na ulimi na midomo miwili? Na Tukambainishia zote njia mbili – (iliyo njema na iliyo mbaya)?"**

Sura 51:56 **"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu."**

Sura 18:7 **"Kwa hakika Tumevifanya vilivyoko juu ya ardhi viwe pambo lake, ili tuwatazame ni nani katika wao (viumbe) wenye vitendo vizuri zaidi."**

## Imani ya Uuungu wa Yesu Kristo

M. Je, Yesu ni Mungu?

C. Ndiyo. Katika Injili, kwa mujibu wa Yohana 1:1 **"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu."**

M. Tumeshakubaliana kuwa kitabu kitakatifu hakitakiwi kiwe kinapingana. Kama kuna aya mbili zinazopingana, basi ni aya moja tu itakayokuwa ni ya kweli au zote mbili ni za uwongo, kwa kuwa zote mbili haziwezi kuwa sahihi. Kwa mujibu wa Yohana 1:1 Yesu ni Mungu. Sasa, kuna miungu mingapi? Kwa uchache miwili. Hili linapingana na vifungu vingi vya Biblia: Kumbukumbu 4:39 **"Kwa hivyo ujue, leo hivi, ukaweka moyoni mwako, ya kuwa BWANA ndiye Mungu katika mbingu juu, na katika nchi chini; hapana mwingine."** Kumbukumbu 6:4 **"Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja."** Isaya 43:10-11 **"... mpate kujua, na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye; kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwepo mwingine."** Isaya 44:6 **"...BWANA wa Majeshi, asema hivi; Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu."** Isaya 45:18 **"Maana BWANA, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu; Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine."**

Kutokana na Isaya 45:18 Tunahitimisha kuwa Mungu peke yake ndiye Muumba na hakuna mwingine, wala Yesu, hajashiriki katika uumbaji.

Pia soma Kumbukumbu 4:35; Kutoka 8:10; 2 Samweli 7:22; 1 Wafalme 8:23; 1 Nyakati 17:20; Zaburi 86:8, 89:6 na 113:5; Hosea 113:4; na Zakaria 14:9.

C. Lakini hayo yote yapo katika Agano la Kale. Je, unayapata maelezo kama hayo katika Agano Jipya?

M. Bila shaka. Soma Marko 12:29, pale palipoandikwa kuwa Yesu mwenyewe amesema: **"Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja."**

1 Wakorintho 8:4 **"... twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu."** 1 Timotheo 2:5 **"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na**

**wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu."** Sasa unaweza kusema kama Yohana 1:1 ni sahihi na aya hizi zote si sahihi, au kinyume chake.

C. Vipi mtu ataweza kufanya maamuzi hayo?

M. Hebu, tulitazame jambo hilo katika mtazamo wa Qurani, ambao unalingana na kile alichokisema Yesu mwenyewe katika Biblia. Yesu ametajwa mara nyingi katika Qurani kama ni **"Neno kutoka kwa Allah."** Katika Sura 3:39: **"Mara Malaika wakamlingania, hali amesimama akisali chumbani, kwamba Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kuwa utazaa mtoto; umwite) Yahya, atakayekuwa mwenye kumsadikisha (Mtume atakayezaliwa) kwa Neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu (naye ni nabii Isa) na atakayekuwa bwana kabisa na mtawa na Nabii anayetokana na watu wema. (Nao ni nyinyi)."**

Katka Sura 3:45 **"(Kumbukeni) waliposema Malaika: "Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kumzaa mtoto bila ya mume, bali kwa kutamkwa) Neno tu litokalo Kwake (la kukwambia 'Zaa' ukazaa pasina kuingiliwa). Jina lake ni Masih, isa, mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu"** Katika aya mbili zote, Yesu anaitwa "Neno kutoka kwa Allah," kwa hiyo inamaanisha ni Neno litokalo kwa Allah au linalomilikiwa na Allah," inalingana na 1 Wakorintho 3:23: **"Nanyi ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu."** Yohana 1:1 ingepaswa iandikwe: **"... na Neno lilikuwa la Mungu."** Huenda kosa limetokea katika kutafsiri kutoka lugha ya Kiarami kwenda Kigiriki, kwa makusudi au si kwa makusudi. Katika lugha ya Kigiriki, Theos ni Mungu, wakati Theou inamaanisha ya Mungu (tazama kamusi yoyote ya Kigiriki au ya Biblia, au kitabu Muhammad katika Biblia na Profesa Abdul Ahad Dawud, askofu wa zamani wa Uramiah, ukurasa 16). Hii tofauti ya herufi moja tu ina matokeo makubwa.

C. Kwa nini Yesu anaitwa "Neno la Mungu" katika vitabu viwili vyote?

M. Kuumbwa kwa Yesu ndani ya fuko la uzazi la Mariamu kulikuwa bila ya mbegu za uzazi za mwanamume, kwa kuwa hilo lilikuwa kwa amri ya Allah: "Kuwa" kama ilivyotajwa katika Sura ya 3:47 **"(Maryamu) akasema: "Mola wangu! Nitapataje mtoto, na hali mtu yoyote hakunigusa?" Akasema (Mola wake): "Ndivyo vivyo: Mwenyezi Mungu huumba Anavyopenda: Anapohukumu jambo, Huliambia: 'Kuwa', (basi) likawa."**

C. Yesu ni Mungu kwa sababu yeye amejazwa Roho Mtakatifu.

Kuna watu wengine waliojazwa Roho Mtakatifu? Je, wote ni miungu? Tazama Matendo 11:24 **"Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani, watu wengi wakaongezeka upande wa Bwana."** Na Matendo 5:32 **"Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio."** Pia unatakiwa usome Matendo 6:5; 2 Petro 1:21; 2 Timotheo 1:14; 1 Wakorintho 2:16; Luka 1:41.

C. Lakini Yesu alijazwa Roho Mtakatifu akiwa tumboni mwa mama yake.

M. Jambo hilo hilo lilikuwa kwa Yohana Mbatizaji, kwani tunasoma katika Luka 1:13-15 **"Lakini yule Malaika akamwambia, Usiogope, Zakaria, maana dua yako imesikiwa, na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yohana....... naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye."**

C. Lakini Yesu alifanya miujiza. Aliwalisha watu elfu moja kwa mikate mitano na samaki wawili tu.

M. Jambo hilo hilo lilifanywa na Elisha na Eliya. Elisha aliwalisha watu mia kwa vipande ishirini vya mikate na mashuke kidogo ya nafaka (ngano), 2 Wafalme 4:44 inasimulia: **"Basi akawaandikia, nao wakala, wakasaza, sawasawa na Neno la BWANA."** Elisha aliongeza mafuta ya mjane, katika 2 Wafalme 4:7 **"... Enenda ukayauze mafuta haya, uilipe deni yako; nayo yaliyosalia uyatumie wewe na watoto wako."** Pia tazama 1 Wafalme 17:16 **"Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la BWANA alilolinena kwa kinywa cha Eliya."** Pia tazama 1 Wafalme 17:6 **"Kunguru wakamletea [Eliya] mkate na nyama asubuhi, na mkate na nyama jioni, akanywa maji ya kile kijito."**

C. Lakini Yesu aliponya ukoma.

M. Elisha alifanya vivyo hivyo, alimwambia Naaman yule Mkoma aoge katika mto Jodani. Kama inavyosimuliwa katika 2 Wafalme 5:14 **"Ndipo akashuka, akajichovya mara saba katika Yordani; sawasawa na neno lake yule mtu wa Mungu [Elisha]; nayo nyama ya mwili wake ikarudi ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto mchanga, akawa safi."**

C. Lakini Yesu alimfanya kipofu aweze kuona tena.

M. Elisha alifanya vivyo hivyo: 2 Wafalme 6:17 **"Elisha akaomba, akasema, Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona. BWANA akamfumbua macho yule mtumishi; naye akaona;...."** 2 Wafalme 6:20 **"Hata walipokwisha kuingia Samaria, Elisha akasema, BWANA wafumbue macho watu hawa, wapate kuona. BWANA akawafumbua macho, wakaona; kumbe! Walikuwa katikati ya Samaria."** Vilevile, Elisha amesemwa kuwa alisababisha upofu: 2 Wafalme 6:18 **"Na walipomtelemkia Elisha akamwomba BWANA, akasema, Uwapige, nakusihi, watu hawa kwa upofu. Akawapiga kwa upofu sawasawa na neno la Elisha."**

C. Yesu alifufua wafu.

M. Linganisha hilo na Eliya: 1 Wafalme 17:22 **"BWANA akaisikia sauti ya Eliya; na roho ya mtoto ikamrudia, akafufuka."** Muujiza kama huo pia ulifanywa na Elisha: 2 Wafalme 4:34 **"Akapanda juu ya kitanda, akajilaza juu ya mtoto, akaweka kinywa chake juu ya kinywa chake, na macho yake juu ya macho yake, na mikono yake juu ya mikono yake; akajinyoosha juu yake; mwili wake yule mtoto ukaanza kupata moto."** Hata kuigusa mifupa ya Eliya kuliweza kufanya wafu wapate uhai: 2 Wafalme 13:21 **"Ikawa walipokuwa wakimzika mtu angalia, waliona kikosi; wakamtupa yule mtu kaburini mwa Elisha; mara yule maiti alipoigusa mifupa ya Elisha, alifufuka, akasimama kwa miguu."**

C. Lakini Yesu alitembea juu ya maji.

M. Musa alinyoosha mkono wake juu ya bahari: Kutoka 14:21-22 **"Musa akanyoosha mkono wake juu ya bahari;... Wana wa Israeli wakaenda ndani kati ya bahari katika nchi kavu; nayo maji yalikuwa ukuta kwao mkono wa kuume, na mkono wa kushoto."**

C. Yesu aliweza kuwafurusha mapepo?

M. Yesu mwenyewe amekiri kuwa watu wengine wanaweza kufanya hilo: Matayo 12:27 na Luka 11:19 **"Na mimi nikitoa pepo kwa Beelzebuli, je! wana wenu huwatoa kwa nini? Kwa sababu hiyo hao ndiyo watakaowahukumu."** Pia wanafunzi wa Yesu waliwatoa mapepo, kama alivyosema Yesu: Matayo 7:22 **"Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?"**

Hata mitume ya uongo ilifanya maajabu, kama ilivyotabiriwa na Yesu mwenyewe: Matayo 24:24 **"Kwa maana watatokea makristo wa**

**uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule."**

C. Lakini Eliya na Elisha walifanya miujiza kwa kumwomba Bwana.

M. Yesu naye alifanya miujiza kwa uweza wa Mungu, kama alivyosema yeye mwenyewe: Yohana 5:30 **"Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka". Na Luka 11:20 "Lakini, ikiwa mimi natoa pepo kwa kidole cha Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia."**

Miujiza yote iliyofanywa na Yesu imeshafanywa na mitume iliyopita, pia wanafunzi wake, na hata makafiri. Kwa upande mwingine, Yesu hawezi kufanya mwujiza kwa makafiri (wasio na imani): Marko 6:5-6 **"Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, ispokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutoamini kwao. Akazunguka-zunguka katika vile vijiji, akifundisha."**

C. Lakini Yesu alifufuka siku ya tatu baada ya kufaliki.

M. Tutazungumzia kusulubiwa kwake baadaye, kwa sababu kuna mabishano mengi sana juu ya hilo. Kwa sasa, nitakachosema ni kuwa, hilo limesemwa na Paulo, ambaye kamwe hajamwona Yesu akiwa hai: 2 Timotheo 2:8 **"Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu, wa uzao wa Daudi kama inenavyo injili yangu."**

Habari ya kufufuliwa katika Marko 16:9-20 nayo imeshaondoshwa katika Biblia nyingi. Kama haijaondoshwa, basi imechapwa kwa maandishi madogo au ndani ya mabano na yakiwa na ufafanuzi. Tazama Revised Standard Version, The New American Standard Bible, na the New World Translation of The Holy Scriptures ya Mashahidi wa Yehova. Hebu nikuulize kitu kimoja: Je, Yesu ameshadai kuwa yeye ni Mungu au ameshasema: "Mimi ni Mungu wenu, niabuduni?"

C. Hapana, lakini yeye ni Mungu na ni mtu.

M. Lakini ameshadai kuwa yeye yupo hivyo?

C. Hapana.

M. Kwa hakika, yeye ameshatabiri kuwa watu watamwabudu yeye bure, wataamini imani isiyoundwa na Mungu bali na mwanadamu: Matayo

15:9 **"Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu."**

Imani zote za Ukristo wa sasa zimeundwa na wanadamu: Utatu, Uungu mwana wa Yesu, Uungu wa Yesu Kristo, na imani ya Dhambi ya Asili na Uwokovu kwa njia ya mateso ya Yesu. Kutokana na maneno ya Yesu mwenyewe yaliyosajiliwa katika Agano Jipya, ni wazi kuwa yeye kamwe hajapatapo kudai Uungu wala kujitambulisha kuwa ni mshirika wa Mungu: **"... na ya kuwa sifanyi neno kwa nafsi yangu.."** Yohana 8:28; **"... kwa maana Baba ni mkuu kuliko mimi.... Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja."** Marko 12:29 **"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"** Marko 15:34 na **"...Ee Baba, mikononi mwako naiweka royo yangu"** Luka 23:46, na **"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala mwana, ila Baba."** Marko 13:32. Yesu alikuwa anaitwa mtume, mwalimu kutoka kwa Mungu, mtumishi Wake, Masihi, na baadaye akaongezewa na kuitwa Mwana wa Mungu, na kisha akawa Mungu Mwenyewe.

Hebu sasa na tutumie akili zetu: Vipi mwanamke anayekufa amzae Mungu? Yesu alilala, wakati Mungu kamwe halali: Zaburi 121:4 **"Naam, hata sinzia wala hata lala usingizi, Yeye aliye mlinzi wa Israeli"** Mungu lazima anakuwa na nguvu zaidi. Lakini, vipi watu walimtundika Yesu na kumsulubu kama inavyodai Biblia? Vipi Yesu atakuwa Mungu kama yeye alimwabudu Mungu (alimwomba) kama viumbe hai vingine: Luka 5:16 **"Lakini yeye alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu akaomba."**

Yesu alijaribiwa na Shetani kwa siku arobaini; Luka 4:1-13, lakini katika Yakobo 1:13 inasema: **"... maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu..."** Sasa, vipi Yesu atakuwa Mungu? Hatuwezi kuona mantiki (akili) zaidi.

C. Ndiyo, mimi mwenyewe sifahamu hilo, lakini tunalazimika kukubali hilo kiupofu.

M. Je, mwelekeo huo haupingani na Biblia yenyewe, inayosema kuwa unalazimika kukithibitisha kitu: 1 Wathesalonike 5:21 **"Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema."**

C. Kwa kweli, hilo linachafua sana.

M. Lakini katika 1 wakorintho 14:33 inasema: **"Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vilevile kama ilivyo katika**

**makanisa yote ya watakatifu."** Imani zilizoundwa na wanadamu zinatengeneza machafuko.

## Imani ya kuamini Uungu Mwana wa Yesu

M. Je, Yesu ni Mtoto wa Mungu?

C. Ndiyo. Soma Matayo 3:17, pale Yesu alipobatizwa na Yohana: **"Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye."**

M. Hutakiwa kulichukua neno "Mwana" kwa maana ya sisisi, kwa sababu Biblia vilevile inawachukulia mitume wengi na watu wengine kuwa ni watoto wa Mungu. Soma Kutoka 4:22

C. **"Nawe umwambie Farao, Bwana asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu."**

M. Hapa ni Yakobo (Israeli) mtoto Wake wa kwanza. Soma 2 Samweli 7:13-14 au 1 Nyakati 22:10.

C. 2 Samweli 7:13-14 **"Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele. Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu..."**

M. Inachanganya zaidi ukisoma Yeremia 31:9 **"... maana mimi ni baba wa Israeli, na Efraimu ni mzaliwa wa kwanza wangu."** Katika Kutoka 4:22, sasa hivi, tumeona Israeli naye ameitwa mtoto wake wa kwanza. Nani hasa, ndiye mtoto wa kwanza: Israeli au Efraimu? Hata watu wa kawaida wanaweza kuwa watoto wa Mungu. Soma Kumbukumbu 14:1.

C. **"Ninyi mmekuwa wana wa BWANA, Mungu wenu."**

M. Watu wa kawaida pia wanaweza kuitwa watoto wa kwanza wa Mungu. Soma Warumi 8:29. **"Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."**

M. Kama wote ni watoto wa kwanza, sasa Yesu atakuwa nani?

C. Yeye ni mtoto wa pekee wa Mungu kwa kuzaliwa.

M. Muda mrefu kabla ya kuzaliwa Yesu, Mungu amemwambia Daudi Zaburi 2:7 **"Nitaihubiri amri, BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa."** Kwa hiyo Daudi vilevile ni Mtoto wa Mungu wa kuzaa. Maana ya "Mwana wa Mungu" si maana ya sisisi ispokuwa ni ya istiari. Nayo inaweza kuwa mtu apendwaye na Mungu. Pia Yesu

amesema kuwa Mungu si Baba yake peke yake lakini pia ni Baba yanu Matayo 5:45, 48.

C. **“ili mpate kuwa wana wa Baba yenu...”** na **“Basi nyinyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.”**

M. Utaona katika vifungu vingi vya Biblia kuwa msemo “Mwana wa Mungu” linamaanisha mapenzi, upendo na ukaribu na Mungu, na hilo si kwa Yesu peke yake. Utaona wana na mabinti wa Mungu: 2 Wakorintho 6:18 **“Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike.”** Kwa mtazamo wa kifungu hiki na vifungu vingine katika Biblia, hakuna mantiki yoyote kwa nini Yesu azingatiwe kuwa ni mwana wa Mungu kwa maana ya sisisi au ufahamu wa pekee.

C. Lakini yeye hana baba. Hiyo ndiyo sababu kuwa yeye ni mwana wa Mungu.

M. Basi unalazimika kumzingatia Adamu kuwa ni mwana wa Mungu, kwa kuwa yeye hana baba wala mama. Katika Luka 3:38, inasema **“...wa Adamu, wa Mungu.”** Soma Waebrania 7:3. **“Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu; huyo adumu kuhani milele.”**

M. Nani huyo? Jibu katika Waebrania 7:1 **“Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu; kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu...”** Yeye ni wa pekee zaidi kuliko Yesu au Adamu. Kwa nini yeye azingatiwi kuwa ni mtoto wa Mungu au Mungu Mwenyewe?

C. Kwa hiyo, Yesu unamwitaje?

M. Waislamu wanamwita Yesu, mtoto wa Mariamu.

C. Hakuna mtu atakayepinga hilo.

M. Ndiyo, hilo ni lepesi na hakuna mtu wa kulikana. Yesu amejiita mwana wa mwanadamu na amekataa kuitwa mtoto wa Mungu. Soma Luka 4:41.

C. **“Pepo nao waliwatoka watu wengi, wakipiga kelele na kusema, Wewe u Mwana wa Mungu. Akawakemea, asiwaache kunena, kwa sababu walimjua kuwa ndiye Kristo”**

M. Ni wazi hapa kuwa alikataa kuitwa mwana wa Mungu. Pia alikataa cheo kama hicho katika Luka 9:20-21, na kuwaambia wanafunzi wake wasi mchukulie kwa njia hiyo.

C. **“Akawaambia, Nanyi mwasema ya kwamba mimi ni nani? Petro akamjibu akasema, Ndiwe Kristo wa Mungu. Akawaonya akawakataza wasimwambie mtu neno hilo.”**

M. Yesu, aliyekuwa Masihi mtarajiwa, mtume, aliongezwa kutoka mwalimu hadi mwana wa Mungu, Bwana, na mwishowe Mungu. Soma Yohana 3:2 **“Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu...”**; Yohana 6:14 **“Basi watu wale, walipoiona ishara aliyoifanya, walisema, Hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimwenguni.”** Pia Yesu aliitwa mtume katika Yohana 7:40; Matayo 21:11; Luka 7:16 na 24:19. Katika Matendo 9:20, tunasoma: **“Mara [Paulo] akamuhubiri Yesu katika masinagogi, ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.”** (Kutokana na haya, pia unaweza kuhitimisha kuwa Wakristo wa mwanzo walikuwa wanatumia masinagogi, lakini baadaye pale Ukristo ulipoacha mafundisho asili ya Yesu, makanisa yakaanzishwa. Paulo, Barnabas, na Mataifa walifurushwa watoke kwenye masinagogi, kwa kuwa walituhumiwa kuwa wamekufuru na kuleta machafuko. Tazama Matendo 13:50, 17:18, na 21:28.). Katika Luka 2:11, inasemekana kuwa: **“Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.”** Na Yohana 1:1 **"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu."**

## Je, Yesu amesulubiwa?

**M.** Qurani inaeleza katika Sura 4:157 kuwa Yesu hakusulubiwa: **“Na kwa (ajili ya) kusema kwao: “Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mungu,” hali hawakumwuua wala hawakumsulubu,...”** Je, unaendelea kuamini kuwa Yesu amefia msalabani?

C. Ndiyo, alikufa na baadaye akafufuka.

M. Sote tunaafikiana kuwa hakuna mtu aliyeshuhudia muda aliofufukia. Wao walilikuta kaburi alilolala Yesu likiwa tupu na wakahitimisha kuwa amefufuka, kwa sababu wanafunzi na mashahidi wengine walimwona akiwa hai baada madai ya kusulubiwa. Je, haiwezekani kuwa, kama inavyodai Qurani, kwamba hajafa msalabani?

C. Ushahidi upo wapi?

M. Hebu tutazame vifungu vya Biblia ambavyo vinaunga mkono hitimisho hilo. Je, unayapa uzito zaidi yale aliyoyasema Yesu au tetesi za wanafunzi, mitume, na mashahidi wengine?

C. Bila shaka, zaidi ni kwa kile alichosema Yesu mwenyewe.

M. Hiyo ni kwa mujibu wa vile alivyosema Yesu: Matayo 10:24 **“Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake.”**

C. Lakini Yesu mwenyewe amesema kuwa atafufuka miongoni mwa wafu: Luka 24:46 **“Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, Kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;”**

M. Kuteseka mara nyingi kunatiwa chumvi zaidi katika Biblia kwa kutumia msamiati wa “kufa,” kama Paulo aliovyosema katika 1 wakorintho 15:31 **“Naam, ndugu, kwa huku kujisifu kwangu nilikonako juu yenu katika Kristo Yesu Bwana wetu, ninakufa kila siku.”** (yaani ninateseka kila siku). Huu ni ushahidi mwengine:

1. Msalabani, Yesu alimsihi sana Mungu amsaidie: Matayo 27:46 **“Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?”** Katika Luka 22:42, inasimuliwa kuwa; **“Akasema, Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke.”** (Kombe hilo ni kombe la mauti.)

2. Ombi la Yesu asife msalabani lilikubaliwa na mungu, kwa mujibu wa Luka, mwandishi wa Waebrania, na Yakobo. Kwa hiyo, vipi afie msalabani? Luka 22:43 **“Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu.”** Hili linamaanisha kuwa malaika amemuhakikishia kuwa Mungu hato mwacha bila ya kumpa msaada: Waebrania 5:7 **“Yeye, siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu.”** Maombi ya Yesu “yalisikilizwa,” jambo linalomaanisha kuwa maombi yake yalijibiwa na Mungu kwa wema: Yakobo 5:16 **“...Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.”** Yesu mwenyewe amesema katika Matayo 7:7-10 **“Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona, bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akiomba samaki, atampa nyoka?”** Ikiwa maombi ya Yesu yote yalikubaliwa na Mungu, likiwemo lile ombi lake asife msalabani, sasa itakuwaje mng`ang`anie kuwa amefia msalabani?

3. Miguu yake haikuvunjwa na askari wa Kirumi: Yohana 19:32-33 **“Basi askari wakaenda, wakamvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulubiwa pamoja naye. Lakini walipomjia Yesu na kuona ya kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu.”** Je, wewe unategemea madai ya askari hao kuwa Yesu alikuwa amekwishakufa, au walitaka kumwokoa kwa kuwa walikuwa wanaamini kuwa Yesu alikuwa hana kosa kabisa?

4. Kama Yesu alifia msalabani, damu yake ingeganda na kwa hiyo kusingekuwa na damu ya kububujika kutoka mwilini mwake pale alipochomwa kitu cha ncha kali. Lakini Injili inaeleza kuwa damu na maji zilitoka: Yohana 19:34 **“Lakini askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara ikatoka damu na maji.”**

5. Mafarisayo walipomtaka Yesu athibitishe kazi yake ya kweli, alijibu: Matayo 12:40 **“Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.”** Bila kujali kipengele cha wakati, ambacho nacho hakikuwa michana mitatu na mausiku matatu bali ilikuwa ni mchana mmoja (Jumamosi, mchana tu) na mausiku mawili (usiku wa Ijumaa na wa jumamosi). Je, Yona alikuwa hai katika tumbo la nyangumi?

C. Ndiyo.

M. Je, Yona aliendelea kuwa hai pale alipotemwa kutoka tumboni mwa nyangumi?

C. Ndiyo.

M. Basi Yesu alikuwa bado yu hai, kama alivyotabiri.

6. Yesu mwenyewe ameeleza kuwa, yeye hajafia msalabani. Mapema, asubuhi ya Jumapili Mariamu Magdalena aliende kaburini, lililokuwa tupu. Alimwona mtu amesimama anayeonekana ni kama mtunza bustani. Baada ya mazungumzo, Magdalena alitambua kuwa huyo alikuwa ni Yesu na akataka kumgusa. Yesu alisema, kama inavyosimuliwa katika Yohana 20:17 **"Yesu akamwambia, Usinishike, kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba..."** "Usinishike" huenda kwa sababu vidonda vya mwilini vingetonesheka na kumuuma. **"Kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba."** Maana yake ni kuwa yeye bado yupo hai, kwa sababu mtu anapokufa anarudi tena kwa Muumba. Huu ulikuwa ni uthibitisho wenye nguvu sana na umekubaliwa na Yesu mwenyewe.

7. Baada ya tuhuma za kusulubiwa, wale wanafunzi walidhani kuwa yule aliyesulubiwa hakuwa ndiye Yesu yule yule kimwili bali kiroho, kwa sababu miili iliyofufuliwa inakuwa "kiroho."

C. Subiri dakika moja. Vipi anahakikisha kuwa miili iliyofufuliwa inakuwa ni ya "kiroho"?

M. Hicho ndicho alichokisema Yesu mwenyewe katika Biblia: kuwa wao ni sawa na malaika.

C. Wapi anaposema hivyo?

M. Katika Luka 20:34-36 **"Yesu akawaambia, Wana wa ulimwengu huu huoa na kuolewa; lakini, wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi; wala hawawezi kufa tena; kwa sababu huwa sawasawa na malaika, nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo."** Kisha Yesu aliwakinaisha kuwa yeye alikuwa ni mtu yule yule kwa kuwaruhusu waguse mikono yake na miguu yake. Kwa kuwa bado walikuwa hawajamwamini, aliwaomba wamletee nyama ili awaonyeshe kuwa yeye bado anakula kama kila kiumbe hai kinavyokula. Soma Luka 24:36-43 **"Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu.**

**Wakashtuka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, mbona mnafadhaika? na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake. Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao."**

8. Kama bado unaamini kuwa alikufa msalabani, basi alikuwa ni mtume wa uwongo na amelaaniwa na Mungu kwa mujibu wa vifungu hivi: Kumbukumbu 13:5 **"Na yule nabii, au yule mwotaji wa ndoto, na auawe..."** Kumbukumbu 21:22-23: **"Akiwa mtu ametenda dhambi ipasayo kufa, akauawa, nawe ukamtundika juu ya mti; mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku iyo hiyo; kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu; usije ukatia unajisi katika nchi yako akupayo BWANA, Mungu wako, iwe urithi wako."**

Kuamini kifo hicho cha msalabani ni kuabisha unabii wake. Wayahudi wanadai kuwa wao wamemuua Yesu msalabani ili kuonyesha kuwa Yesu ni nabii wa uwongo. Wakristo wanaamini kuuliwa msalabani, ni lazima kwa ajili ya imani yao ya kuokolewa dhambi na, matokeo yake, wanalazimika waamini kulaaniwa kwa Yesu, vilevile. Imani hii ya Kikristo inapingana na mafundisho ya Biblia katika Hosea 6:6 **"Maana nataka fadhili wala si sadaka; na kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa."** Pia inapingana na mafundisho ya Yesu mwenyewe katika Matayo 9:13 **"Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka..."** Yesu amesema tena katika Matayo 12:7 **"Lakini kama mngalijua maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msingaliwalaumu wasio na hatia."**

C. Sasa, kwa nini watu wanaamini ufufuo?

M. Paulo ndiye aliyefundisha ufufuo: Matendo 17:18 **"...Wengine [Wayahudi] wakasema, Mpuzi huyu [Paulo] anataka kusema nini? Wengine walisema, Anaonekana kuwa mtangaza habari za miungu migeni, kwa maana alikuwa akihubiri habari za Yesu na ufufuo."** Paulo ambaye hajamwona Yesu, vilevile alikiri kuwa ufufuo wa Yesu ni Injili yake 2 Timotheo 2:8 "**Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu, wa uzao wa Daudi kama inenavyo injili yangu.**" Vilevile Paulo alikuwa ni mtu wa kwanza kutangaza kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu: Matendo 9:20 **"Mara [Paulo] akamuhubiri Yesu katika**

**masinagogi, ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.”** Kwa hiyo, Ukristo si mafundisho ya Yesu bali ya Paulo.

C. Lakini Marko 16:19 inaeleza kuwa Yesu alipaa mbinguni na kukaa kuumeni kwa Mungu: **“Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.”**

M. Kama nilivyokwambia pale mwanzoni, kuwa Marko 16:9-20, imeshafutwa katika Biblia maalumu: The Revised Standard Version, The New American Standard Bible na the New World Translation of The Holy Scriptures of the Jehovah`s Witnesses Church. Kama bado unaamini kuwa Yesu ni mungu kwa kuwa alinyanyuliwa mbinguni, kwa nini hukubali uungu wa mitume wengine walionyanyuliwa mbinguni?

C. Walikuwa akina nani hao?

M. Eliya: 2 Wafalme 2:11-12 **“... naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. Naye Elisha akaona, akalia, ... Asimwone tena kabisa...”** Naye Henoko alichukuliwa na Mungu kwenda mbinguni: Mwanzo 5:24 **“Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana mungu alimtwaa.”** Hilo pia, lilirudiwa katika Waebrania 11:5 **“Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu.”**

## Imani ya Mateso, Kifo cha Yesu na Dhambi ya Asili

**C. K**wa hiyo wokovu wa dhambi kwa kupitia kusulubiwa kwa Yesu haukuwa sehemu ya mafundisho ya Yesu?

M. Imani ya kuamini Mateso na Kifo cha Yesu kuwa ni wokovu, imekubaliwa na Kanisa baada ya karne tatu au nne tangu kuondoka kwa Yesu na kuicha dunia hii. Imani hii inapingana na Biblia, kama vinavyyoonyesha vifungu vifuatavyo: Kumbukumbu 24:16 **"Mababa wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao; kila mtu na auawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe."** Yeremia 31:30 **"Bali kila mtu atakufa kwa sababu ya uovu wake mwenyewe...",** Ezekieli 18:20 **"Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe; haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake."** Adamu na Hawa walibeba majukumu ya dhambi yao wenyewe, liyosamehewa na Allah kwa mujibu wa kitabu cha Uislamu.

C. Lakini hayo yapo katika Agano la Kale.

M. Soma kile alichokisema Yesu mwenyewe katika Matayo 7:1-2

C. **"Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa."**

M. Soma 1 Wakorintho 3:8.

C. **"Basi yeye apandaye, na yeye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu zake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe."** Lakini sisi tunaamini Dhambi ya Asili!

M. Je, bado unanitaka nikuthibitishie kuwa watoto wanazaliwa bila ya kuwa na dhambi? Soma Matayo 19:14.

C. **" Lakini Yesu akasema, Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao."**

M. Kwa hiyo kila mtu anazaliwa bila dhambi na watoto wote ni miliki ya ufalme wa mbinguni. Je, unajua kuwa, alikuwa ni Paulo aliyekomesha sheria ya Musa? Soma matendo 13:39.

C. **“Na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.”**

M. Hebu nikuulize swali. Kwa nini unaamini ufufuo ikiwa Paulo mwenyewe, ambaye kamwe hajamwona Yesu akiwa hai, amekiri kuwa hilo lilikuwa ni la injili yake?

C. Hilo limeandikwa wapi?

M. Soma 2 Timotheo 2:8.

C. **"Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu, wa uzao wa Daudi kama inenavyo injili yangu."** Lakini kwa nini tunalazima kuamini kuwa amesulubiwa na akafufu baada ya kufa?

M. Sijui ni kwa nini. Uislamu, ambao ni mafundisho ya mitume ya Mungu yote, kamwe haujapatapo kuchafuliwa na imani au ufahamu utokao katika upagani na ushirikina.

C. Hicho ndicho ninachokitafuta.

M. Kwa nini usitamke shahada au ushuhuda, kwanza kwa Kingereza na kisha kwa Kiarabu. Acha nikusaidie kuitamka.

C. Nashuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah, Asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mtumishi wake na ni nabii wake. Ashhadu an la illaha illa Allah, wahdahu la sharikah lahu, wa ashhadu anna Muhammad abduhu wa rasuluhu.. Je, mtume Muhammad ametajwa katika Biblia?

M. Ndiyo, lakini si lazima kwa Mwislamu kujua hilo kutoka katika Biblia. Kwa vile wewe umeshaisoma Biblia, ningependelea kujadiliana nawe juu ya hilo kwa ufupi mara nyingine.

Tazama: Majadiliano yaliyosalia yataendeshwa baina ya Waislamu wawili: “M” na “m.”

# MUHAMMAD KATIKA BIBLIA

## Isamili Na Isaka Wote Wawili Waribarikiwa

M. Kwa nini Ismaili na mama yake Hajiri waliondoka na kumwacha Sara?

m. Baada ya kuachishwa ziwa Isaka, mama yake ambaye ni Sara alimwona Isamaili akimdhihaki Isaka. Baada ya hapo, Sara hakumtaka Ismaili arithi pamoja na mwanawe Isaka: Mwanzo 21:8-10 **"Mtoto akakua, akaachishwa kunyonya; Ibrahimu akafanya karamu kuu siku ile Isaka alipoachishwa kunyonya. Sara akamwona Yule mwana wa hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka."**

M. Isaka alikuwa na umri wa miaka miwili pale alipoachishwa ziwa. Kwa hiyo, Ismaili alikuwa na umri wa miaka kumi na sita, kwa sababu Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka themanini na sita pale Hajiri alipomzaa Ismaili na alikuwa na umri wa miaka mia moja pale alipozaliwa Isaka, kwa mujibu wa Mwanzo 16:16 **"Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka themanini na sita, hapo Hajiri alipomzalia Abramu Ishmaeli."** Na Mwanzo 21:5 **"Naye Ibrahimu alikuwa mtu wa mika mia, alipozaliwa mwana wake Isaka."** Mwanzo 21:8-10 hiyo inapingana na Mwanzo 21:14-21, pale Ismaili aliposimuliwa kuwa ni mtoto wa kuwekwa mabegani kwa mama yake, alipoitwa "mama" na "mwana," pale wote wawili walipomwacha Sara **"Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa Hajiri akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika jangwa la Beer-sheba..."** hayo ni maelezo ya yanayomuhusu mtoto mchanga, si mwenye miaka kumi na tatu hadi kumi na tisa (teenager). Kwa hiyo Isamaili na mama yake Hajiri walimwacha Sara muda mrefu kabla ya kuzaliwa Isaka. Kwa mujibu wa maandiko ya Kiislamu, Ibrahimu alimchukua Ismaili na Hajiri na walifanya makazi mapya huko Maka, panapoitwa Parani ndani ya Biblia (Mwanzo 21:21) Kwa sababu ya maelekezo ya matakatifu aliyopewa Ibrahimu ikiwa ni sehemu ya mpango wa Mungu. Hajiri alikimbia mara saba baina ya vijilima viwili, Safa na Marwa, akitafuta maji. Hii ni asili ya moja ya ibada ifanywayo wakati wa hija huko Maka. Kisima cha maji kilichotajwa katika Mwanzo 21:19 bado kipo na kinajulikana kwa jina la Zamzam. Wote wawili Ibrahimu na Ismaili baadaye, waliijenga Kaaba ndani ya Maka. Eneo alilolitumia Ibrahimu kuswalia karibu na Kaaba

bado lipo na linajulikana kwa jina Maqam Ibrahimu, yaani, Kituo cha Ibrahimu. Wakati wa hija, mahujaji walio Maka na Waislamu wa dunia nzima wanaadhimisha sadaka ya Ibrahimu na Ismaili kwa kuchinja wanyama.

m. Lakini Biblia inataja kuwa Isaka ndiye alikuwa wa kutolewa muhanga.

M. Kitabu cha Uislamu kinaeleza kuwa agano lilifanywa kati ya Mungu, Ibrahimu, na mwanawe wa pekee Ismaili, na lilifanyika pale Ismaili alipotakiwa kutolewa muhanga. Katika siku kama hiyo, Ibrahimu, Ismaili, na wanaume wote wa nyumba ya Ibrahimu walitahiriwa. Wakati huo, Isaka hajazaliwa: Mwanzo 17:24-27 **"Naye Ibrahimu alikuwa mwenye umri wa miaka tisini na kenda alipotahiriwa nyama ya govi lake. Na Ishmaeli mwanawe alikuwa mtu wa miaka kumi na mitatu, alipotahiriwa nyama ya govi lake. Siku ile akatahiriwa Ibrahimu na Ishmaeli mwanawe. Na watu wote wa nyumba yake, wazaliwa nyumbani, na wanunuliwa kwa fedha katika mkono wa mgeni, wakatahiriwa pamoja naye."**

Mwaka mmoja baadaye, alizaliwa Isaka, na alitahiriwa pale alipokuwa na siku nane: Mwanzo 21:4-5 **"Ibrahimu akamtahiri Isaka mwanawe, alipokuwa mwenye siku nane, kama Mungu alivyomwamuru. Naye Ibrahimu alikuwa mtu wa miaka mia, alipozaliwa mwana wake Isaka."** Kwa hiyo pale agano lilipofanywa na kufungwa (kutahiriwa na kutolewa muhanga) Ibrahimu alikuwa na miaka tisini na tisa na Ismili kumi na tatu. Isaka alizaliwa mwaka mmoja baadaye, pale Ibrahimu alipokuwa ana umri wa miaka mia moja.

Wajukuu wa Ismaili, akiwemo Mtume Muhmmadi, na Waislamu wote, bado wanatekeleza agano la kutahiriwa hadi leo. Katika swala zao tano za kila siku, Waislamu wanajumuisha dua kwa Ibrahimu na kizazi chake pamoja na dua kwa Muhammad na kizazi chake.

m. Lakini katika Mwanzo 22 imetajwa kuwa ni Isaka aliyekuwa wa kutolewa muhanga.

M. Najua, lakini utaona mgongano wa hapo. Imetaja **"mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka."** Je, hiyo haikutakiwa iwe "mwana wako wa pekee, umpendaye, Ismaili," kwani Ismaili ndiye alikuwa na miaka kumi na tatu na isaka hajazaliwa? Alipozaliwa Isaka, Ibrahimu alikuwa na watoto wawili. Kwa sababu ya upendeleo pofu, jina Ismaili lilibadilishwa likawa Isaka katika Mwanzo 22 yote. Lakini Mungu amelikinga neno "wa pekee" ili kutuonyesha kile kilichotakiwa kiwepo.

Hilo neno "...nitauzidisha uzao wako..." katika Mwanzo 22:17, mwanzoni lilinasibiana na Ismaili katika Mwanzo 16:10. Je, haikuwa kwa Mwanzo 22 inafaa kutumika kwa Ismaili? **"Mimi nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa"** imesharudiwa mara mbili kwa ismaili katika Mwanzo 17:20 na Mwanzo 21:18, na kamwe haijatumika kwa Isaka hata kidogo.

m. Wayahudi na Wakristo wanaendeleza madai kuwa Isaka alikuw ni mbora zaidi kuliko Ismaili.

M. Wanaweza kusema hivyo kama watakavyo, lakini Biblia haiungi mkono madai hayo: Mwanzo 15:4 **"Nalo neno la BWANA likamjia likinena, Huyu hatakurithi, bali atakayetoka katika viungo vyako ndiye atakayekurithi."** Kwa hiyo Ismail naye pia alikuwa ni mrithi wa Ibrahimu.

Mwanzo 16:10 **"Malaika wa BWANA akamwambia, hakika nitakuzidishia uzao wako, wala hautahesabika kwa jinsi utakavyokuwa mwingi."**

Mwanzo 17:20 **"Na kwa habari za Ishmaeli nimekusikia, nimembariki, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu."**

Mwanzo 21:13 **"Naye mwana wa mjakazi nitamfnya kuwa taifa, maana huyu naye ni uzao wako."**

Mwanzo 21:18 **"Ondoka, akamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako, kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa."**

Kumbukumbu 21:15-17 **"Akiwa mtu yuna wake wawili, mmoja ampenda, mmoja hampendi, nao wamemzalia watoto, ampendaye na asiyempenda wote wawili; na yule mzaliwa wa kwanza akiwa ni wa mke asiyependwa; ndipo itakapokuwa ya kwamba siku atakayowarithisha wanawe alivyo navyo, asimweke mwana wa ampendaye kuwa mzaliwa wa kwanza mbele ya mwana wa asiyempenda, naye ndiye mzaliwa wa kwanza huyu; lakini amkubali mzaliwa wa kwanza mwana wa yule asiyempenda, kwa kumpa mafungu mawili katika vyote alivyo navyo; kwa maana ndiye mwanzo wa nguvu zake; haki ya mzaliwa wa kwanza ni yake yeye."** Uislamu haupingi baraka za Mungu kwa Isaka na kizazi chake, lakini mtoto wa ahadi ni Ismaili, ambaye kutoka kwake ameibuka Muhammad akiwa ni mtume wa mwisho.

m. Lakini Wakristo na Wayahudi wanadai kuwa Ismaili alikuwa ni mtoto wa haramu (nje ya ndoa).

M. Hilo ndilo walisemalo, lakini silo lielezwalo na Biblia. Vipi mtume mkuu kama Ibrahimu awe na mke wa kinyume cha sheria na mtoto wa nje ya ndoa!

Mwanzo 16:3 **"... Sarai... akampa Abramu mumewe, [Hajiri] awe mkewe."** Kama ndoa ilikuwa ya halali, vipi mtoto wao awe wa haramu? Je, ndoa baina ya wageni wawili, Mkaldawo na Mmisri, si halali kuliko ndoa baina ya mwanamume na binti wa baba yake? Hata kama ni uwongo dhidi ya Ibrahimu au si uwongo, hilo limeelezwa katika Mwanzo 20:12 **"Naye kweli ni ndugu yangu, binti wa baba yangu ila siye mwana wa mama yangu, ndipo akawa mke wangu."**

Pia, Jina Ismaili lilichaguliwa na Allah Mwenyewe: Mwanzo 16:11 **"Malaika wa BWANA akamwambia, tazama! Wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Ishmaeli, maana BWANA amesikia kilio cha mateso yako."** Ismaili maana yake "Mungu anasikia." Ni wapi katika Biblia palipoandikwa kuwa Ismaili ni mtoto wa haramu?

m. Hakuna sehemu yo yote.

M. Muda mrefu kabla ya kuzaliwa Ismaili na Isaka, Allah alifanya agano na Ibrahimu: Mwanzo 15:18 **"...akasema Uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huo mto mkubwa, mto Frati."** Je, eneo kubwa la arabuni halipo kati ya mto Nile na Frati, sehemu ambayo kizazi chote cha Ismaili kilifanya makazi hapo baadaye?

m. Je, unamaanisha kuwa hakuna ardhi aliyoahidiwa Isaka na kizazi chake?

M. Sisi Waislamu hatupingi kuwa Isaka vilevile alibarikiwa. Tazama Mwanzo 17:8 **"Nami nitakupa wewe na uzao wako baada yako nchi hii unayoikaa ugeni, nchi yote ya Kanaani, kuwa milki ya milele, nami nitakuwa Mungu wao."**

Je**,** vilevile, unaona tofauti ya kuwa Ibrahimu aliitwa "mgeni" katika Kanaani lakini si katika ardhi iliyopo baina ya Nile na Frati? Akiwa ni Mkaldawo, alikuwa ni karibu zaidi na Uwarabu kuliko Uyahudi.

m. Lakini lile agano lilifanywa kwa Isaka, kwa mujibu wa Mwanzo 17:21 **“Bali agano langu nitalifanya imara kwa Isaka, ambaye Sara atakuzalia majira kama haya mwaka ujao.”**

M. Je, hilo linamtoa Ismaili? Wapi katika Biblia panaposema kuwa Allah hakufanya agano lolote na Ismaili?

m. Hakuna sehemu yoyote.

## Kigezo cha Mtume na Yeremia

Yeremia 28:9 **"Nabii atabiriye habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa BWANA amemtuma kweli kweli."**

Neno Islamu pia linamaanisha utulivu na amani, amani kati ya Muumba na viumbe vyake. Utabiri huu wa Yeremia hauendani na Yesu, kwa kuwa Yesu mwenyewe ameeleza kuwa hajaja kwa amani: Luka 12:51-53 **"Je! Mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia, La, sivyo, bali mafarakano. Kwa kuwa tokea sasa katika nyumba moja watakuwamo watu watano wamefarakana, watatu kwa wawili, wawili kwa watatu. Watafarakana baba na mwanawe, na mwana na babaye; mama na binti yake, na binti na mamaye; mkwe mtu na mkwewe, mkwe na mkwe mtu."** Pia tazama matayo 10:34-36.

### Hadi atakapokuja Shiloh (Yeye Mwenye Amani)

Huu ulikuwa ujumbe wa Yakobo kwa watoto wake kabla hajafariki: Mwanzo 49:1 **"Yakobo akawaita wanawe, akasema, Kusanyikeni, ili niwaambie yatakayo wapata siku za mwisho."**

Mwanzo 49:10 **"Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, Wala mfanya sheria kati ya miguu yake, Hata atakapokuja Yeye** *[katika Biblia za Kingereza limeandikwa neno 'Shiloh']*, **mwenye milki, Ambaye mataifa watamtii."**

Shiloh pia ni jina la mji, lakini maana yake ya hakika ni amani, utulivu, kupunzika (Islamu). Neno hilo haliwezi kuwa linakusudiwa mji kwa hapa. Kama linakusudiwa mtu, litakuwa ni Shaluah (Elohim), lililofisidiwa, yaani Mtume (wa Allah).

Kwa hiyo mitume ya Kiisraeli katika mlolongo wa ukoo wa Isaka utakoma punde tu akija Shiloh. Hii inalingana na Sura 2:133 **"Je; (nyinyi Mayahudi na Manasara) mlikuwapo yalipomfikia Yaaqubu mauti, alipowaambia wanawe: "Je, mtamuabudu nani baada yangu?" Wakasema: "Tutamwabudu Mola wako na Mola wa baba zako, Ibrahimu na Ismaili na Is-haqa; Mungu mmoja tu, na sisi tunanyenyekea Kwake."** [kwa Kiarabu 'muslimuuna = Waislamu/wenye kujisalimisha]**"**

Mabadiliko ya utume kwenda kwa taifa lingine yalitishiwa katika Yeremia 31:36 **"Amri hizi zikiondoka, zisiwe mbele zangu, asema BWANA, ndipo wazao wa Israeli nao wataacha kuwa taifa mbele**

**zangu milele."** Hili pia liliashiriwa na Yesu katika Matayo 21:43 **"Kwa sababu hiyo nawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake."**

### Baka ni Maka

Kaaba tukufu, iliyojengwa na Ibrahimu na mwanawe Ismaili, ipo Maka. Jina hili Maka limetajwa mara moja katika Qurani Sura 48:24. Jina lingine la Maka ni Baka, kulingana na lahaja za kikabila. Pia jina hili Baka nalo limetajwa mara moja, katika Sura 3:96 **"Kwa yakini nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya ibada) ni ile iliyoko Makka [kwa kiarabu imeandikwa Bakkah] yenye baraka na uwongozi kwa ajili ya walimwengu wote."** Ni jambo la kushangaza kiasi cha kutosha, hili neno Baka lilitajwa na Mtume Daudi katika Zaburi yake 84:6 **"Wakapita kati ya *bonde la Vilio*** *[Baca]*,[9] **Hulifanya kuwa chemchemi. Naam, mvua ya vuli hulivika baraka."** Hiyo chemchemi hapa ni ile chemchemi ijulikanayo kama chemchemi ya Zamzam, ambayo bado ipo hadi leo katika eneo lilokaribu na Kaabah.

Formatted: Font color: Blue

[9] Katika Kingereza imeandikwa Baca na hili neno si la kingereza, inasemekana ni la Kiebrania lenye maana ya kilio, vilio, sasa kama ni hivyo nalo neno baka kwa Kiarabu lina maana ya kilio, pia usisahau kuwa lugha za Kiarabu na Kiebrania zina maneno yanayofanana na kuwa na maana moja.

## Nyumba ya Utukufu Wangu

Isaya 60:-

1. **"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, N a utukufa wa BWANA umekuzukia."** 60:1 Linganisha haya na Sura 74:1-3 **"Ewe [Muhammad] uliyejifunika maguo. Simama uonye (viumbe). Na Mola wako umtukuze."**
2. **"Maana, tazama, giza litafunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabila za watu; Bali BWANA atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako."** 60:2 Kuja kwa Mtume Muhammad kulikuwa wakati wa giza pale dunia iliposahau upweke wa Mungu kama ulivyofundishwa na Ibrahimu na mitume mingine yote. Akiwemo Yesu.
3. **"Na mataifa wataijiria nuru yako, Na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako."** 60:3.
4. **"Inua macho yako, utazame pande zote; Wote wanakusanyana; wanakujia wewe; Wana wako watakuja kutoka mbali, Na binti zako watabebwa nyongani."** 60:4 Ndani ya miaka ishirini na mitatu Warabu wote waliungana.
5. **"Ndipo utakapoona na kutiwa nuru, Na moyo wako utatetemeka na kukunjuka; Kwa kuwa wingi wa bahari utageuzwa kukujia, Utajiri wa mataifa utakuwasilia."** 60:5 Ndani ya karne moja, Uislamu ulienea nje ya mipaka ya Uarabuni.
6. **"Wingi wa ngamia utakufunika, Ngamia vijana wa Midiani na Efa; Wote watakuja kutoka Sheba; Wataleta dhahabu na uvumba; Na kuzitangaza sifa za BWANA."** 60:6.
7. **"Makundi yote ya Kedari yatakusanyika kwako, Kondoo waume wa Nebayothi watakutumikia; Watapanda juu ya madhabahu yangu ya kibali, Nami nitaitukuza nyumba ya utukufu wangu."** 60:7 Makabila ya Kedar (Warabu) waliotawanyika, waliungana. "Nyumba ya utukufu wangu." Hapa inarejea kwa Nyumba ya Allah ya Maka na sio Kanisa la Kristo kama inavyofundishwa na wazungumzaji wa Kikristo. Ni ukweli kwamba vijiji vya Kedari (kwa uchache, sasa ni Saudia Arabia yote) navyo vipo katika nchi ya pekee duniani iliyobakia bila kujipenyeza kwa ushawishi wa Kanisa.

11. **"Malango yako nayo yatakuwa wazi daima; hayatafungwa mchana wala usiku; Ili watu wapate kukuletea utajiri wa mataifa, Na wafalme wao wakiongozwa pamoja nao."** 60:11 Ni ukweli kwamba huo msikiti uliozunguka Kaabah mjini Maka umeendelea kuwa wazi mchana na usiku tangu pale Mtume

Muhammad alipoondosha masanamu yaliyokuwepo ndani yake kiasi cha karne kumi na nne zilizopita. Watawala na raia wameshaenda kufanya hija.

## Mpanda Punda na Mpanda Ngamia

Mtazamo wa Isaya juu ya wapandaji wanyama wawili katika Isaya 21:7 **"Naye akiona kundi la wapanda farasi, wakienda wawili wawili, na kundi la punda, na kundi la ngamia;..."**

Nani aliyekuwa mpanda punda? Kila mwanafunzi wa Shule za Jumapili anamjua mtu huyo kuwa alikuwa ni Yesu: Yohana 12:14 **"Naye Yesu alikuwa amepata mwana-punda, akampanda, kama vile ilivyoandikwa."**

Nani, basi, aliyeahidiwa kuwa ni mpanda ngamia? Huyu mtume mwenye nguvu sana hajagunduliwa na wasomaji wa Biblia. Mtu huyo ni Mtume Muhammad. Kama hili halikubaliani naye, basi utabiri huo bado haujatimizwa. Hii ndiyo sababu Isaya ametaja katika 21:13 **"Ufunuo juu ya Arabuni..."** inamaanisha majukumu ya Waislamu wa Kiarabu, na bila shaka kwa sasa ya Waislamu wote, kueneza ujumbe wa Uislamu.

Isaya 21:14 **"Waleteeni wenye kiu maji, Enyi wenyeji wa nchi ya Tema, Nendeni kuwalaki wakimbiao na chakula chao."** Tema huenda ni Madina, alipohamia Mtume Muhammad na wafuasi wake. Kila mhamiaji aliunganishwa na mkazi wa Madina kwa muungano wa udugu, na Mtume. Pia wahamiaji walipewa chakula na makazi.

Isaya 21:16 **"Kwa sababu Bwana ameniambia hivi, Katika muda wa mwaka, kama miaka ya mtu mwenye kuajiriwa, utaangamia utukufu wote wa Kedari."** Sawasawa kabisa, katika mwaka wa pili Hijiria (kuhama), wapagani walishindwa katika vita vya Badri.

Mwisho kabisa Isaya 21:17 inahitimisha na **"...hao mashujaa wa Kedari watakuwa wachache; maana BWANA, Mungu wa Israeli, amenena neno hili."** Kedar ni mtoto wa pili wa Ismaili (Mwanzo 25:13), na kutoka kwake, hatimaye, aliibuka Mtume Muhammad. Mwanzoni watoto wa Kedari walimshambulia Muhammad na wafuasi wake. Lakini kwa kuwa wengi wao waliukubali Uislamu, idadi ya watoto wa Kedari walio wapinzani wa Kipagani iliaanza kupungua. Katika baadhi ya aya za Biblia, "Kedar" ni kisawe cha "Arab" kwa ujumla, kama ilivyo katika Ezekieli 27:21 **"Arabuni, na wakuu wote wa Kedari..."**

## Mtume Kama Musa

Mungu alimhutubia Musa: Kumbukumbu 18:18 **"Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, mimi nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawambia yote nitakayomwamuru."**

1 .Miongoni mwa ndugu za Israeli wa (kizazi cha Ibrahimu kupitia Isaka) ni wana wa Ismaili (kizazi cha Ibrahimu kupitia Ismaili). Hapa Yesu ameondoshwa, kwa kuwa yeye ni Mwiisraeli. Vinginevyo ingetakiwa iandikwe "mtume miongoni mwenu."

2 .Je, Muhammad si kama Musa? Kama hili halikubaliki, basi ahadi hii bado inatakiwa ikamilishwe. Jedwali hapo chini, limechukuliwa kutoka katika Al-ittihad (Januari – Machi 1982), ukurasa 41, huo ni ufafanuzi binafsi:

Hapa chini, ni mlinganisho baina ya sifa muhimu sana kati ya Musa, Muhammad na Yesu ambazo huenda zikabainisha utambulisho wa "mtume huyo" aliyekuwa aje baada ya Musa:

| Eneo la kulinganishwa | Musa | Muhammad | Yesu |
|---|---|---|---|
| Kuzaliwa: | Kawaida | Kawaida | Si kawaida |
| Maisha ya kifamilia: | Ameoa na ana watoto | Ameoa na ana watoto | Hajaoa wala hana watoto |
| Kifo: | Kawaida | Kawaida | Si kawaida |
| Kazi: | Mtume/Kiongozi wa nchi | Mtume/Kiongozi wa nchi | Mtume |
| Kuhamishwa kwa nguvu (ukubwani kwake): | Kaelekea Median | Kaelekea Madina | Hajahama |
| Kukabiliana na maadui: | Alikimbizwa/fukuzwa kwa nguvu | Alifukuzwa kwa nguvu/Vita | Hakuna kukabiliana |
| Matokeo ya makabiliano: | Ushindi wa Kiroho na Kimwili | Ushindi wa Kiroho na Kimwili | Ushindi wa Kiroho |
| Kuandikwa kwa Ufunuo: | Wakati wa uhai wake (Torati) | Wakati wa uhai wake (Qurani) | Baada yake |
| Tabia ya mafundisho: | Kiroho/Sheria | Kiroho/Sheria | Kwa kiasi kikubwa ni Kiroho |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kukubaliwa uongozi wake (na watu wake) | Alikataliwa, kisha akakubaliwa | Alikataliwa, kisha akakubaliwa | Alikataliwa (na Wayahudi wengi) |

Formatted: Font color: Blue

3. "Nitatia maneno yangu kinywani mwake." Ufunuo wa Mungu ulikuja kupitia Gabrieli, na fikra binafsi za Mtume Muhammad hazikuhusika. Lakini hili linaafikiana na ufunuo mtakatifu wote. Labda hili limetajwa hapa maalumu kwa sababu ya kulinganishwa na ufunuo wa Musa, unaoaminika kuwa "uliandikwa katika majedwali."

Kumbukumbu 18:19 **"Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake."**

Katika Qurani, Sura 113 miongoni mwa Sura zake 114 zinaanza na kifungu: **"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu."** Kifungu hiki vilevile ni kifungu cha kawaida kwa maongezi ya kila siku ya Mwislamu, kwa vile kinatumiwa pale yanapoanza matendo mapya. Aya hiyo 'si kwa jina la Mungu', bali "kwa jina langu" "Jina halisi la Mungu ni Allah." Halina ujinsia wala wingi, kama uliopo katika neno la Kingereza "God." Wakristo wanaanza kwa "Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

Pia inatakiwa itazamwe kuwa wale wote watakao kuwa hawasikilizi au kukubali ujumbe utakaouleta wataadhibiwa. Hili linalingana na Sura 3:19 **"Bila shaka Dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu..."** na Sura 3:85 **"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)."**

## Mtumishi, Mjumbe na Mteule wangu

Ukamilisho wa wazi wa utabiri wa Muhammad unapatikana katika Isaya 42:1

1. **“Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia roho yangu juu yake; naye atawatolea mataifa hukumu.”** Pia anaitwa “Mjumbe wangu” katika aya ya 19. Hapana shaka kuwa mitume yote kwa hakika walikuwa ni watumishi, wajumbe, na wateule wa Allah. Ndiyo, hakuna mtume, mwenye sifa za pekee kama Muhammad, ulimwenguni anayeitwa kwa jina hili la pekee. Kwa Kiarabu ni: Abduhu wa Rasuluhu Mustapha (Mtumishi wake na mjumbe wake.) Ushuhuda wa mwenye kuukubali Uislamu ni: “Ninashuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah, hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mtumishi wake na ni mjumbe wake.” Mfumo huo huo unakaririwa mara tano kwa siku, katika adhana ya swala kabla ya kuanza kwa kila swala, mara tisa kwa siku katika tashahudi za swala zote za lazima, na mara nyingine nyingi kama Mwislamu anatekeleza swala yoyote ya nyongeza (swala za sunna). Jina maarufu zaidi la Mtume Muhammad ni Rasul Allah, linalomaanisha “Mjumbe wa Allah.”

2. **“Hatalia, wala hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu.”** Hili linaelezea adabu ya Mtume Muhammad.

3. **“...atatokeza hukumu kwa kweli.”**

4. **“Hatazimia, wala hata kata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani; na visiwa vitaingojea sheria yake.”** Hili lilinganishwe na Yesu, ambaye hajawashinda maadui zake na kusikitishwa kwa sababu ya kukataliwa na Waisraeli.

5. 6-- **“Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya mataifa.”** Ibara “na kukulinda” inaashiria kuwa hakuna mtume mwengine atakayekuja baada yake. Kwa muda mchache mataifa mengi yaliingia Uislamu.

6. **“Kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa.”** “Macho ya vipofu, maisha ya kiza” inamaanisha wapagani na upagani wao. **“kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa.”** Inamaanisha kukomesha utumwa kwa mara ya kwanza katika historia ya wanadamu.

7. 8-- **“Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.”** Mtume Muhammad ni wa kipekee miongoni mwa mitume yote, kwa maana, yeye ni “mtume wa mwisho” na mafundisho yake yamebakia bila kubadilishwa hadi leo, kama utalinganisha na Ukristo na Uyahudi.

8. 10-- **“Mwimbieni BWANA wimbo mpya, Na sifa zake tokea mwisho wa dunia...”** Nyimbo mpya, kama ilivyo si ya Kiebrania wala Kiarama, bali ya Kiarabu. Sifa za Mungu na mjumbe wake Muhammad zinaimbwa mara tano kila siku katika minara ya misikiti na mamilioni ya misikiti dunia nzima.

9. 11-- **“Jangwa na miji yake na ipaze sauti zao, Vijiji vinavyokaliwa na Kedari; Na waimbe wenyeji wa Sela, Wapige kelele toka vilele vya milima.”** Katika Mlima Arafa ulio karibu na Maka, mahujaji wanaimba yafuatayo kila mwaka: “Nimekuitika, Ee Allah. Nimekuitika. Nimekuitika. Huna mshirika. Nimekuitika. Hakika shukurani zote ni zako, baraka na ufalme ni wako. Huna mshirika. “Isaya 42 kamwe haiwezi kukubaliana na mtume yoyote wa Kiisraeli, kwa kuwa Kedari ni mtoto wa pili wa Isamili. Tazama Mwanzo 25:13.

10. 12-- **“Na wamtukuze BWANA, na kutangaza sifa zake visiwani.”** Ni hakika, Uislamu umesambaa hadi katika visiwa vidogo vya mbali hadi Indonesia na visiwa vya bahari ya Karebiani.

11. 13-- **“...Atawatenda adui zake mambo makuu.”** Kwa muda mfupi, Ufalme wa Mungu ardhini ulisimikwa kwa kuja Muhammad. Hii Sura ya 42 ya Isaya inakubaliana na sifa za Mtume Muhammad kisawasawa.

## Mfalme Daudi Alimwita Huyo “Bwana Wangu”

Zaburi 110:1 **“Neno la BWANA kwa Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwafanyapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako.”**

Kuna mabwana wawili waliotajwa hapa. Ikiwa Bwana wa kwanza (mzungumzaji) ni Mungu, Bwana wa pili (mzungumziwa) naye kamwe hawezi kuwa ni Mungu, kwa kuwa Daudi anamjua Mungu mmoja tu. Kwa hiyo ingekuwa inasomeka: “Mungu amemwambia Bwana wangu,...” Nani aliyeitwa na Daudi “Bwana wangu”? Kanisa litasema Yesu. Lakini hili limekataliwa na Yesu mwenyewe katika Matayo 22:45, Marko 12:37, na Luka 20:44. Yeye amejitoa mwenyewe kukiacha cheo hicho, kwa kuwa alikuwa ni mwana wa Daudi. Vipi Daudi atamwita yeye “Bwana wangu” kama yeye alikuwa ni mtoto wake, kama alivyodai hivyo. Yesu amesema, katika Luka 20:42-44 **“Maana, Daudi mwenyewe asema katika chuo cha zaburi, Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwaweke adui zako, Kuwa kiti cha kuwekea miguu yako. Basi Daudi amwita Bwana; amekuwaje mwana wake?**” Yesu lazima angetoa jibu na si nukuu za Injili nne. Hata hivyo, imetajwa kwa uwazi katika Injili ya Barnabas kuwa ahadi ilitolewa kwa Ismaili, si kwa Isaka. Bwana huyo wa Daudi alikuwa ni Muhammad, aliyemwona kiroho. Hakuna mtume aliyetimiza vigezo hivyo zaidi ya Muhammad. Hata kazi za mitume yote kwa pamoja zinabakia kuwa ni ndogo ukizilinganisha na ile ya Muhammad ambaye, kwa kipindi cha miaka ishirini na mitatu, aliweza kuacha urithi (Uislamu) ambao unabakia bila kubadilishwa mpaka sasa.

### Wewe U Nabii Yule?

Wayahudi waliwatuma makuhani na Walawi kwenda kwa Yohana Mbatizaji wamuulize yeye ni nani hasa. Yohana 1:20-21 **“Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba, Mimi siye Kristo. Wakamwuliza, Ni nini basi? U Eliya wewe? Akasema, Mimi siye. Wewe u nabii yule? Akajibu, La.”**

Swali la muhimu sana hapa ni: Wewe u nabii yule? Nani aliyekuwa mtume aliyesubiriwa kwa muda mrefu ambaye alitakiwa aje baada ya kuja kwa Yesu na Yohana Mbatizaji? Je, hakuwa ni yule kama Musa (Kumbukumbu 18:18) ambaye ni Muhammad?

## Kubatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto

Matayo 3:11 **“Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto.”**

Kama Yesu amedokezwa hapa, Yohana Mbatizaji asingelazimika kurudi tena na kuishi jangwani, lakini angemng`ang`ania na kuwa mmoja wa wanafunzi wake, jambo ambalo hakulifanya. Kwa hiyo hapa, Yohana alikuwa anadokeza juu ya mtume mwingine mwenye nguvu sana. Yule ajaye baada Yohana Mbatizaji hawezi kuwa ni Yesu, kwa kuwa wote walikuwepo wakati mmoja. Kwa mara nyingine tena, je, huyo hakuwa ni Mtume Muhammad aliyeashiriwa na Yohana Mbatizaji?

### Mdogo Katika ufalme wa Mbinguni

Yesu amenukuliwa, katika Matayo 11:11, akisema **“Amin, nawaambieni, hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye.”**

Je, unaweza kuamini kuwa Yohana Mbatizaji ni mkuu kuliko Adamu..., Ibrahimu, Musa, Daudi, na mitume wengine wengi? Wapagani wangapi waliobatizwa na Yohana Mbatizaji, na alikuwa na wafuasi wangapi? Lakini hii si nukta kuu. Swali: Nani aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni, na ni mkuu kuliko Yohana Mbatizaji? Bila shaka si Yesu, kwa kuwa wakati huo ufalme wa mbinguni ulikuwa bado haujaundwa na kwa hiyo kamwe hajadai kuwa yeye ni mdogo, yaani, mdogo kiumri kuliko wote. Ufalme wa mbinguni unajumuisha Mungu akiwa ndiye Mkuu na mitume yote. Mdogo au mwenye umri mdogo kwa hapa ni Mtume Muhammad.

## Heri Wapatanishi

Katika hotuba yake ya mlimani, Yesu alinukuliwa, katika Matayo 5:9, akisema **“Heri wapatanishi; Maana hao wataitwa wana wa Mungu.”**

Moja ya maana za neno “Uislamu” ni amani: amani baina ya Muumba na wenye kuabudu. Yesu hawezi kukusudia kuwa kazi yake ilikuwa ni mpatanishi, kama alivyoeleza kwa uwazi kuwa yeye hakutumwa kwa lengo hilo (Matayo 10:34-36): **“Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga. Kwa maana nilikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake.”** Pia tazama Luka 12:49-53.

## Msaidizi

Yohana 14:16 **“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele.”**

Sisi kwa hakika hatujui neno asili la Kiarama lilotumiwa na Yesu kwa “Comforter, Msaidizi.” Biblia nyingine zinatumia “Consoler,” “Advocate,” “Helper,” na katika Biblia ya Kigiriki tunakuta neno “Paraclete.” Kuna fafanuzi mbalimbali kwa neno hilo, miongoni mwazo ni “Roho Mtakatifu” na “Neno.”

Qurani inaeleza katika 61:6 kuwa Yesu kwa uwazi kabisa ametaja jina Ahmadi: “Na (wakumbushe) aliposema (Nabii) Isa bin Mariamu (kuwaambia Mayahudi): **“Enyi wana wa Israili! Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na kutoa habari njema ya Mtume atakayewajia nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. (Muhammad. Na maana yake majina mawili yote haya ni moja. Maana yake mwenye kushukuriwa kwa maneno yake mazuri na vitendo vyake vizuri na kila chake, kwani vyake vyote ni vizuri). Lakini alipowajia kwa hoja zilizo wazi, walisema: “Huu ni udanganyifu uliyo dhahiri.”**

Vyo vyote itakavyokuwa tafsiri ya Msaidizi (Comferter), tunahitimisha kuwa Yesu ameondoka bila ya kumaliza kazi na kuna mtu anakuja kukamilisha kazi yake. Acha tupime, kwa mwangaza wa Biblia, kama huyu Msaidizi analingana na tabia za Mtume Muhammad:

1. **“Msaidizi mwingine”**: Wasaidizi wengi wameshakuja, na mwingine atakuja.

2. **“Ili akaye hata milele”**: Kwa kuwa hakukuwa na haja ya mwingine aje baada yake, na alikuwa ni mtume wa mwisho. Mafundisho yatabakia milele na kubakia salama. Kwa hakika, Qurani na mafundisho yote ya Mtume Muhammad yamebakia kama yalivyokuwa kwa miaka 1400 iliyopita.

3. **“Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi...”** (Tazama Yohana 16:8) Mitume mingine yote, hata Ibrahimu, Musa, Daudi, na Suleimani waliwatiadabu majirani zao na watu wao kwa dhambi zao, lakini si ulimwengu, kama alivyofanya Muhammad. Yeye si tu aling`oa mizizi ya kuabudu masanamu huko Arabuni ndani ya kipindi cha miaka ishirini na mitatu, lakini pia alipeleka wajumbe kwa Heraclius, mtawala wa Persian na himaya ya Warumi, kwa Najashi (mfalme wa Ethiopia), na kwa Muqauqis (Gavana wa Misri). Yeye aliwakemea

Wakristo kwa kuugawa umoja wa Mwenyezi Mungu kuwa ni wa sehemu tatu, na kwa kumnyanyua Yesu kuwa Mwana wa Mungu na kisha kuwa Mungu mwenyewe. Alikuwa ni Muhammad aliyewakemea Wayahudi na Wakristo kwa kuharibu vitabu vyao, amedhihirisha haki ya kuzaliwa ya Ismaili, na kuwasafisha mitume na tuhuma za uzinzi, ngono za ndugu kwa ndugu, ubakaji, na kuabudu masanamu.

4. **“...yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha hukumiwa.”** Yohana (16:11). Huyu ni Shetani kama ilivyofafanuliwa katika Yohana 12:31 na 14:30. Kwa hiyo Mtume Muhammad amekuja kuutia adabu Ulimwengu kwa hukumu.

5. **“Roho wa kweli”** Yohana (16:13). Tangu utotoni, Mtume Muhammad alikuwa akiitwa Al-Amin, yaani Mkweli Mwaminifu. Mtu huyu pia atakuja na, **“atawaongoza awatie kwenye kweli yote;...”** Yohana (16:13).

6. **“Kwa maana hata nena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena...”.** Yohana (16:13).Qurani ni maneno ya Mungu. Hakuna hata neno moja kutoka kwa Muhammad au Wafuasi wake liloingizwa katika Qurani. Malaika Jibrili (Gabrieli) alimsomea Mtume; naye akaikariri, na kuandikwa na waandishi wake. Maneno yake mwenyewe na mafundisho yake yalisajiliwa katika Hadithi.

Linganisha haya na Kumbukumbu 18:18: **“...mimi nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawambia yote nitakayomwamuru.”** Haya yanalingana na Sura 53:2-4: **“Kwamba mtu wenu (huyu Nabii Muhammad) hakupotea (kwa ujinga) wala hakukosa, (na hali ya kuwa anajua); Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi (ufunuo), uliofunuliwa (kwake).”**

7. **"Na mambo yajayo atawapasha habari yake."** Yohana (16:13). Utabiri mwingi wa Mtume Muhammad umshatokea, na uliobakia utakamilka siku zijazo.

8. **“Yeye atanitukuza mimi...”** Yohana 16:14. Kwa hakika, Qurani na Mtume Muhammad wanamheshimu sana Yesu kuliko inavyofanya Biblia na Wakristo wenyewe. Yafuatayo yatadhihirisha nukta hii:

a. Kuamini kifo cha Yesu msalabani kunashusha hadhi ya utume wake, kwa mujibu wa Kumbukumbu 13:5 **"Na yule nabii, au yule mwotaji wa ndoto, na auawe...”** Pia inambandika laana, (Mungu aepushie mbali hilo!) kwa mujibu wa Kumbukumbu 21:22-23: **“...kwani aliyetundikwa**

**amelaaniwa na Mungu; usije ukatia unajisi katika nchi yako akupayo BWANA, Mungu wako..."**

b. Matayo 27:46 **"...Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"** Je, Yesu angesema maneno kama hayo? Hata asiye mtume angetabasamu kwa mateso hayo, kwa kuwa alijua kuwa kifo chake kingempatia cheo cha shahidi (mfia dini). Je, hili si tusi kwa Yesu na kumpiga kijembe kuwa hakuwa na imani kwa Allah?

c. Sisi Waislamu hatuwezi kuamini kuwa Yesu angewaita Mataifa kuwa ni mbwa na nguruwe na kumtambulisha mama yake kwa neno "mwanamke," kama inavyoeleza Qurani katika Sura 19:32: **"Na (ameniusia) kumfanyia mema mama yangu: wala hakunifanya niwe jeuri, muovu."** Matayo 7:6: **"Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe..."** Yohana 2:4: **"Yesu akamwambia, *Mama*[10] tuna nini mimi nawe?..."**

---

[10] Kwa Kingereza inaonesha wazi kasema ¨woman¨ yaani mwanamke lakini sijui inakuwaje imetafsiriwa mama!

## Ufunuo kwa Mtume Muhammad

Ufunuo wa kwanza wa Allah ni (Sura 96:1-5) kwa kupitia malaika Jibrilu kwenda kwa Muhammad nao ulikuwa neno ‘Iqra’, linalomaanisha “soma.” Kwa kuwa yeye alikuwa hajui kusoma wala kuandika, naye alijibu: “Siwezi kusoma.” Huu ufunuo wa kwanza ulitabiriwa katika Isaya 29:12: **“Kisha chuo hiki apewa mtu asiye na maarifa, akaambiwa, Kisome hicho tafadhali, akasema, Sina maarifa mimi.”**

Aya za Qurani hazikufunuliwa kwa mpangilio kama uliopo katika Qurani. Kwa ibara nyingine, kifungu cha kwanza kufunuliwa si cha ukurasa wa kwanza na kifungu cha mwisho kufunuliwa si ukurasa wa mwisho. Hiyo ni kuwa ufunuo huu umekuja kidogo kidogo na ulikuwa unaingizwa kwenye mpangilio maalumu katika Qurani kama ulivyopangwa na Allah hili nalo limetajwa na Isaya 28:10-11: **“Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo. La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa.”** Lugha nyingine hapa ina maana lugha nyingine (siyo Kiebrania wala Kiarama, bali Kiarabu).

Waislamu wa dunia nzima wanatumia lugha moja, “Kiarabu” katika kumwabudu Mungu wao, katika swala zao, hija, na maamkizi yao wao kwa wao. Umoja huu wa kilugha pia ulitabiriwa katika Sefania 3:9: **“Maana hapo ndipo nitakapowarudisha mataifa lugha iliyo safi, wapate kuliitia jina la BWANA, wamtumikie kwa nia moja.”** Ukweli umekwishakuja kwa Kiarabu, lakini baadhi ya watu wanatarajia Mtume Yesu, kuwa huenda atafundisha wanadamu wamwabudu Allah kwa lugha moja pale atakapokuja kwa mara ya pili. Sisi Waislamu tunahakika kuwa Mtume Yesu, katika ujio wake wa mara ya pili, atawaunganisha Waislamu misikitini mwao, kwani yeye ni kama Mwislamu mwingine: ametahiriwa, hali nguruwe, na answali akiwa na udhu, na kuwa naye anasimama, kurukuu (kuinama kwa unyenyekevu), na kusujudu wakati wa swala zake.

## Marejeo


1. Explanatory English Translation of Holy Qur`an, by Dr. Muhammad TaquiDin al-Hilali na Dr. Muhammad Muhsin Khan.
2. The Holy Bible (King James Version), authorized 1611.
3. The Holy Bible (Revised Standard Version).
4. The New World Translation of the Holy Scriptures (Jehovah1s Witnesses Church).
5. New American Standard Bible.
6. The Myth of Cross, by A. D. Ajijola.
7. The Cross and the Crescent, by Maulana Muhammad Imran.
8. Davis Dictionary of the Bible, 1980.
9. The International Standard Bible Encyclopedia.
10. Smithi`s Bible Dictionary, 1980.
11. The Encyclopedia Britannica, 1980.
12. Muhammad in the Bible, by Prof. Abdul Ahad Dawud.
13. Muhammad in the Bible, by Ahmed Deedat.
14. Jesus: A Prophet of Islam, by Sulaiman Shahid Mufassir.
15. Biblical Studies fromMuslim Perspectives, by S. Mufassir.
16. Muhammad in the Bible, by Jamal Badawi: Al-Ittihad (January-March 1982). 1 Wakati ni desturi kuvua viatu msikitini, kuna suna ya kusali na viatu. (Tazama Sunan Abuu Dawood).
17. Qurani Takatifu – Iliyofasiriwa na Marehemu Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy, aliyekuwa Kadhi mkuu wa Kenya.
18. The Holy Bible in Swahili 1952 Union Version, Swahili Union Bible (1952 edition) UBS 35M 2007.
19. Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili toleo la tatu (TUKI).